# MWINGILIANOMATINI KATI YA *MKAGUZI MKUU WA SERIKALI* NA *MSTAHIKI MEYA*

**NA**

**BOSIRE T. BOSIBORI**

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA IDARA YA KISWAHILI YA**

**CHUO KIKUU CHA NAIROBI**

**2016**

## UNGAMO

Tasnifu hii ni kazi yangu mwenyewe na haijatolewa kwa mahitaji ya shahada katika chuo kikuu kingine chochote.

___________________ __________________

Bosire Teresa Bosibori
C50/67081/2013
(Mtahiniwa) Tarehe

Tasnifu hii imetolewa kutahiniwa kwa idhini yetu tukiwa wasimamizi wa kazi hii tulioteuliwa na Chuo Kikuu cha Nairobi.

___________________ ____________________

Dkt. Evans Mbuthia Tarehe
(Msimamizi)

___________________ ___________________

Dkt. Amiri Swaleh Tarehe
(Msimamizi)

# TABARUKU

Tasnifu hii ninaitabarukia mume wangu mpendwa Stephen Anyona. Amejitolea mhanga kuhakikisha kuwa nimekamilisha elimu yangu.Vilevile, sitasahau watoto wangu: Edith, Brian na Hope ambao wamenivumilia kwa muda ambao sikuweza kushirikiana nao kwa mambo mengi waliponihitaji. Ninatumai kuwa wataweza kutambua umuhimu wa masomo katika maisha ya binadamu.

## SHUKRANI

Safari ndefu huanza kwa hatua moja. Hakika safari hii imekuwa ndefu tangu nilipoanza kozi hii. Imekuwa safari yenye panda shuka nyingi ambazo singeweza kukwepa peke yangu. Siwezi kujigamba na kudai kuwa jitihada zangu pekee zingenipa ufanisi pasipo mchango wa wengine wengi. Nitakuwa ninadanganya nisipowatambua walionisaidia nilipojikwaa na kunihimiza dhidi ya kukata tamaa.

Kwanza kabisa, ninamshukuru Rabuka kwa kunipa siha njema na nguvu za kukamilisha kozi hii. Bila yeye singefika nilipofika.

Shukrani zangu za pekee ni kwa wasimamizi wangu wawili, Dkt. Evans Mbuthia na Dkt. Amir Swaleh. Wamekuwa zaidi ya walimu wangu. Wasomi hawa wameshirikiana nami kama ndugu na sahibu wa karibu. Sitasau ushauri wao daima dawamu. Mola awabariki.

Wahadhiri katika idara ya Isimu na Lugha katika Chuo Kikuu cha Nairobi wanastahiki shukrani chungu nzima. Mchango wao wa moja kwa moja umenisaidia pakubwa sana katika maisha ya masomo yangu. Kuna mambo mengi ambayo singeyajua nisingekutana nao. Miongoni mwao ni pamoja na: Prof. Kineene wa Mutiso, Prof. John Habwe, Prof. Mwenda Mbatia, Prof. Rayya Timammy, Prof. Iribe Mwangi, Dkt. Amir Swaleh, Dkt. Evans Mbuthia, Dkt. Jefwa Mweri, Dkt. Zaja Omboga na Dkt. Ayub Mukhwana.

Ninawashukuru wanafunzi ambao tuliabiri dau la masomo pamoja hadi ufuoni nao ni Agnes Muchiri, Silveria Njeri, Emily Mosota, Lydia Nyambeki, Chepkorir, Kemunto, Faith na Winnie. Asanteni kwa kunifaa katika mijadala na kwa ushauri. Ninawaombea ufanisi katika kila hali maishani.

Ninatoa shukurani zangu kwa mume wangu bwana Stephen Anyona. Amekuwa sahibu wa karibu wa kunishauri maji yalipozidi unga. Isitoshe, alikuwa mwepesi wa kutumwa nilipohitaji msaada wa mbali. Asante sana mume wangu. Maulana akujalie mema duniani.

Ninawashukuru ndugu zangu Marion, Benuel, Collins, Annastasia, Kevin na Barongo kwa mawaidha yao yaliyonisongesha hatua kadha.

Labda sikuweza kutaja kila mmoja aliyenifaa kwa njia moja au nyingine. Kwenu nyote nasema asante sana.

# YALIYOMO

Ungamo .......... ii

Tabaruku .......... iii

Shukrani .......... iv

Yaliyomo .......... v

Ikisiri .......... viii

## SURA YA KWANZA

1.1 Usuli wa mada .......... 1

1.2 Tatizo la utafiti .......... 1

1.3 Madhumuni ya utafiti .......... 2

1.4 Nadharia tete .......... 2

1.5 Sababu za kuchagua mada .......... 3

1.6 Upeo na mipaka ya utafiti .......... 4

1.7 Msingi wa kinadharia .......... 4

1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada .......... 7

1.9 Mbinu za utafiti .......... 9

## SURA YA PILI: MWANDA WA KI- MWINGILIANO KATIKA FASIHI

2.1 Utangulizi .......... 11

2.2 Vipengele vya mwanda wa kimwingilianomatini katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya.* .......... 11

2.3 Msuko .......... 11

2.3.1 Msuko mkuu .......... 12

2.3.2 Msuko kinzani .......... 12

2.3.3 Msuko msago .......... 12

2.3.4 Msuko kioo .......... 12

2.3.5 Msuko rudufu .......... 12

2.4 Wahusika .......... 13

2.4.1 Usawiri wa wahusika ........................................................................................ 14
2.4.2.1 Mbinu za kuwasawiri wahusika ............................................................ 14
2.4.2.2 Maelezo au maneno ya wahusika wengine ............................................ 14
2.4.2.3 Mbinu ya matendo au matumizi ya mazungumzo .................................... 15
2.4.2.4 Mbinu ya majazi ................................................................................. 15
2.4.2.5 Maelezo ya msimulizi au mwandishi ...................................................... 15
2.4.2.6 Mbinu ya mwingilianomatini ................................................................ 16
2.5 Dhamira na maudhui ............................................................................... 16
2.6 Mandhari ............................................................................................... 17
2.7 Vipengele vingine vya kimwingilianomatini ............................................... 18
2.8 Hitimisho ............................................................................................... 19

**SURA YA TATU**: **MSUKO NA MWINGILIANOMATINI**

3.1 Utangulizi ............................................................................................... 20
3.2 Msuko katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* .................................................. 20
3.3 Msuko katika *Mstahiki Meya.* ................................................................ 24
3.4 Hitimisho ............................................................................................... 27

**SURA YA NNE**: **MWINGILIANOMATINI KATIKA UHUSIKA NA MANDHARI**

4.1 Utangulizi ............................................................................................... 28
4.2 Mwingilianomatini katika uhusika ............................................................. 29
4.2.1 Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya ......................................................... 29
4.2.2 Diwani II na Bw. Huruma ...................................................................... 35
4.2.3 Diwani I na Bw. Hakimu ....................................................................... 36
4.2.4 Dida naYosif ........................................................................................ 38
4.2.5 Askari .................................................................................................. 39
4.2.6 Dhiki ya wafanyikazi na wafanyibiashara ................................................ 39
4.2.7 Ghlestakovu na Bili ............................................................................. 40

4.3 Mandhari .......... 41

4.4 Hitimisho .......... 42

**SURA YA TANO: MWINGILIANO WA KIMAUDHUI**

5.1 Utangulizi .......... 44

5.2 Uongozi mbaya .......... 44

5.3 Ukosefu wa uwajibikaji .......... 48

5.4 Unafiki .......... 51

5.5 Ufisadi .......... 54

5.6 Uchafuzi wa mazingira .......... 55

5.7 Migogoro .......... 56

5.8 Utabaka .......... 57

5.9 Hitimisho .......... 59

**SURA YA SITA: HITIMISHO**

6.1 Utangulizi .......... 60

6.2 Muhtasari wa matokeo .......... 60

6.3 Hitimisho .......... 62

6.4 Mapendekezo .......... 62

**MAREJELEO** .......... 64

# IKISIRI

Tamthilia ya Kiswahili ni mojawapo ya tanzu za Fasihi Andishi ya Kiswahili. Tanzu nyingine ni pamoja na riwaya, ushairi, hadithi fupi, novela na zinginezo. Utanzu wa tamthilia umedhihirisha kwa njia moja au nyingine uhusiano wa kimwingilianomatini. Utafiti huu umelenga kuchunguza na kuchanganua mwingilianomatini kati ya tamthilia za *Mstahiki Meya* (Arege,2009) na *Mkaguzi Mkuu wa serikali* (Gogol,1979). Katika kuhakiki hayo, tumetumia nadharia ya Mwingilianomatini iliyoasisiwa na mwana nadharia wa Kifaransa Julia Kristeva. Tumeongozwa na malengo matatu ya utafiti-kuchunguza jinsi tamthilia zinavyoingiliana kifani na kimaudhui vilevile kuchunguza iwapo nadharia ya Mwingilianomatini inafaa katika uhakiki wa tamthilia ya Kiswahili. Utafiti umeongozwa na maswali yafuatayo: Je, tamthilia hizi zina mwingiliano au la, zikiwa zinao, basi kwa kiwango gani? Je, ni sehemu zipi za tamthilia zinaingiliana kwa mujibu wa mwanda wa mwingilianomatini? Kutokana na utafiti huu, imebainika wazi kwamba tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* zinaingiliana katika vipengele vya msuko, usawiri wa wahusika, mandhari na maudhui. Maswali yetu ya utafiti yamepata kujibiwa kikamilifu kwa kuwa tumeweza kuonyesha jinsi tamthilia zinavyoingiliana na kuchangizana. Hatimaye, tumetoa mapendekezo kwa watakaofanya tafiti za baadaye kuhusiana na swala la kuingiliana kwa matini.

# SURA YA KWANZA

## 1.1 Usuli wa mada

Fasihi kama sanaa nyingine yoyote ile ni chombo chenye misingi yake katika ubunifu. Vilevile tamthilia ni aina ya sanaa inayotumia lugha ili kuendeleza tajriba za binadamu (Njogu na chimerah 1999). Fasihi inaweza kuwa simulizi au andishi. Fasihi andishi ina tanzu zake kuu ambazo ni riwaya, hadithi fupi, ushairi na tamthilia. Tamthilia ni mchezo wa kuigiza ambao una wahusika wanaotenda na kuzungumza. Waigizaji huiga matendo ya watu halisi katika jamii. Uigizaji huo hulenga kuwasilisha wazo fulani katika jamii.

Utafiti huu umeshughulikia mwingilianomatini kati ya tamthilia mbili za waandishi waliobobea katika uandishi wa kazi za kifasihi. Waandishi tutakaowaangazia ni Nikolai Gogol na Timothy Arege. Waandishi hawa wameandika kazi nyingi. Nikolai Gogol anasifika kwa uandishi wake wa michezo ya vichekesho iliyokuwa na mianzo yake katika *Order of Vladmir, The Servant's Room, A Lawsuit, A Fragment* na *Government Inspector*.

Kwa upande mwingine, tuna Timothy Arege ambaye mchango wake katika kuendeleza fasihi ni wa kuenziwa. Baadhi ya vitabu vyake ni: *Chamchela* (2007), *Mstahiki Meya* (2009) na *Kijiba cha Moyo* (2009).

Hata hivyo, katika utafiti huu tumejikita katika tamthilia zao mbili *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Gogol) *na Mstahiki Meya (*Arege). Tumechunguza jinsi tamthilia hizi zinavyoingiliana na kuchagizana. Utafiti wetu unanuia kudhihirisha wazi kuwa; binadamu wote ulimwenguni aghalabu hughasiwa na maswala sawa. Aidha waandishi wa kazi za fasihi huweza kulelewa katika mazingira tofauti yaani ya Kiafrika au ya Ulaya lakini wakaandika matukio yayo hayo kwa njia zinazolandana. Tatu, kuonyesha thamani ya kazi hizi kwa kuchunguza namna zinavyoingiliana.

Utafiti wetu umeongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini ambayo inahusishwa na mwananadharia na Kifaransa Julia Kristeva. Aidha tumetalii vipengele anuwai katika mwanda wa kimwingilianomatini kama maandalizi ya kimsingi ya kuhakiki tamthilia hizi mbili zinavyohusiana.

## 1.2 Tatizo la utafiti

Mwingilianomatini ni swala la kimsingi katika fasihi kwa sababu jamii za binadamu

huathiriwa na maswala tofauti ambayo ni ya kijumla kama vile utawala, maadili na mengine mengi. Kwa hivyo si ajabu kazi tangulizi za kifasihi zikaonekana kukaribiana na kazi zingine za baadaye. Swala hili limechunguzwa na wasomi kadha ambao wamedhihirisha kuwa baadhi ya matini za kifasihi huhusiana kwa njia moja au nyingine. Uhusiano huu hupatikana katika tanzu zote za fasihi zikiwemo riwaya, tamthilia, ushairi na kadhalika.

Katika tasnifu hii, tumetafiti mwingilianomatini kati ya tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ya Nikolai Gogol *na Mstahiki Meya* ya Timothy Arege. Tumehakiki vipengele anuwai vya kimwingiliano kama vile: ploti, mandhari, maudhui, na wahusika. Tumechagua mada hii kwa kuwa tamthilia hizi hazijawahi kufanyiwa uhakiki kwa mwelekeo sawa na wetu. Utafiti wetu umeongozwa na maswali yafuatayo: Je, tamthilia hizi mbili zina mwingiliano wa matini au la? Zikiwa zinao, basi kwa kiwango gani? Je, ni sehemu zipi za tamthilia zinaingiliana kwa mujibu wa mwanda wa mwingilianomatini? Je, kuna tofauti zozote zinazojitokeza katika tamthilia hizi kwa jumla? Haya ndiyo maswala tutakayojaribu kuyashughulikia katika tasnifu yetu.

### 1.3 Madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya utafiti huu ni :

i. Kuchunguza jinsi tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Mkaguzi Mkuu* wa *Serikali* zinavyoingiliana kifani.

ii. Kuchunguza jinsi tamthilia hizi zinavyoingiliana kimaudhui.

iii. Kuchunguza iwapo nadharia ya Mwingilianomatini ina utendakazi muhimu katika uhakiki wa tamthilia ya Kiswahili.

### 1.4 Nadharia tete

Utafiti huu umeongozwa na nadharia tete zifuatazo:

i. Baadhi ya matini za kifasihi huchangizana na kuingiliana kifani.

ii. Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu* wa *Serikali* na *Mstahiki Meya* zinaingiliana kimaudhui na kidhamira.

iii. Nadharia ya Mwingilianomatini inafaa katika kuhakiki baadhi ya tamthilia za Kiswahili.

## 1.5 Sababu za kuchagua mada

Tamthilia hizi hazijawahi kufanyiwa utafiti kwa mwelekeo huu wa kuchunguza mwingilianomatini kati yazo. Kwa maoni yetu inafaa kuitumia nadharia hii katika kuhakiki tamthilia za Kiswahili ili kuchangia katika kuziba pengo hili ambalo watafiti wengine hawajalishughulikia.

Waandishi hawa wawili wameandika tamthilia zao katika vipindi tofauti; *Mstahiki Meya (*2009) na *Mkaguzi Mkuu wa Serikali (*1834) tafsiri ya Christon Mwakasaka (1979) lakini kazi hizi zinadhihirisha mwingiliano wa kiwango fulani kama vile inavyodhihirika katika kazi hii. Swala la waandishi kuchangizana na kuingiliana katika kazi zao za kisanaa limekuwepo tangu zamani kama inavyodhihirika katika kazi mbalimbali za kifasihi.

Nadharia ya Mwingilianomatini haijatumiwa sana katika uchanganuzi wa fasihi ya Kiswahili. Hii ni kinyume na nadharia zingine ambazo zimechangiwa na wataalamu wengi. Ni kutokana na jambo hili tumeonelea kuwa kuna umuhimu wa kuitumia ili kuonyesha utendakazi wake katika uhakiki wa fasihi ya Kiswahili.

Vipengele mbalimbali kama vile wahusika, maudhui na ploti huingiliana kujengana na kukamilishana. Ni katika muktadha huu wa kujengana, kukamilishana na kuingiliana ambapo tungetaka kudhihirisha jinsi kazi hizi mbili zinavyoingiliana na kuchangizana.

Katika utafiti huu, tumeamua kushughulikia kazi za waandishi wawili waliokulia katika mazingira na tamaduni tofauti. Nia yetu ikiwa ni kutaka kuonyesha kuwa binadamu wote ulimwenguni aghalabu hukerwa na takribani maswala yanayofanana na aidha waandishi wanaweza kulelewa katika mazingira na tamaduni zinazotofautiana lakini wakaandika mambo yayo hayo kwa njia zinazolandana.

*Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (1834) na *Mstahiki Meya* (2009) zimechaguliwa kuwakilisha vipindi tofauti vya kihistoria ili kuonyesha namna mwingilianomatini unavyoweza kujitokeza katika vipindi tofauti vya kihistoria.

## 1.6 Upeo na mipaka ya utafiti

Kazi za waandishi waliokulia katika mazingira tofauti huweza kuingiliana kwa njia moja au nyingine katika kipengele kimoja au zaidi kwa kuwa waandishi huchota malighafi yao kutoka jamii.

Ni katika misingi hii ambapo tunachunguza mwingiliano kati ya *Mstahiki Meya* (Timothy Arege) na *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* (Nikolai Gogol). Utafiti huu haujashughulikia vipengele vyote katika mwanda wa kimwingilianomatini. Tumechunguza tamthilia hizi kwa mujibu wa vipengele vifuatavyo vya kimwingilianomatini : ploti, mandhari, uhusika na maudhui.

## 1.7 Msingi wa kinadharia

Utafiti huu umeongozwa na nadharia ya Mwingilianomatini. Nadharia hii imepata kufasiriwa na kuhusishwa na wataalamu wengi kama vile De Saussure (1917), Kresteva (1969) na Bakhtin (1981). Saussure anafafanua swala la ishara katika lugha. Naye Bakhtin anajulikana kama mtaalamu aliyezua mtazamo mahsusi wa lugha uliosaidia wengine kuzua nadharia ya Mwingilianomatini. Tofauti na Saussure, Bakhtin alijihusisha na ishara katika lugha na jinsi zinavyoungana ili kuwa na maana. Allen (2000) anaendeleza maoni ya Bakhtin. Yeye alijishughulisha na miktadha ya jamii ambapo maneno yanatumika. Anasisitiza kuwa mahusiano ya maneno yanategemea mahali au mandhari katika jamii, sajili mahususi za kijamii na aidha wakati mahususi wa kutamka na kupokewa kwa maneno.

Hata hivyo, Julia Kristeva ndiye anayesifika kuwa mwanzilishi wa nadharia ya Mwingilianomatini katika miaka ya sitini. Aliendeleza maoni ya Saussure kuhusu jinsi ishara hupata maana katika muundo wa matini na ya Bakhtin ya maneno na maana katika miktadha ya kijamii. Julia anaamini kuwa hamna matini yoyote ile ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake au kujitegemea. Anasisitiza kuwa lazima kuwe na matini nyingine inayohusiana nayo kwa mfano katika mtindo wa kiashiriaji, katika matumizi ya sitiari, tashbihi, taswira na istiara, dhamira, maudhui, muundo wa msuko na usawiri wa wahusika.

Wamitila (2002:136) anasema kuwa kazi yoyote ile huwa na maana kwa sababu mambo fulani yanayohusiana nayo yamekwisha kuandikwa tayari. Kwa hivyo, upokezi na uelewaji wa utanzu kama riwaya unategemea kuwako kwa riwaya nyingine kabla ya

riwaya maalum inayochunguzwa. Kwa mujibu wa mtazamo huu, kazi yoyote ile huwa na maana kwa sababu mambo fulani yanayohusiana nayo yamekwisha kuandikwa tayari. Hata hivyo, mtazamo huu haumaanishi kuwa kazi nyingine huwa zimenukuu zile zilizotangulia bali kazi hizo huchangia katika msimbo fulani ambao unarahisisha vipengele fulani vya uashiriaji. Hii haina maana kuwa kazi fulani itakuwa imenukuu nyingine. Mwingilianomatini sio nadharia ya uchunguzi wa vyanzo au athari za kazi fulani ila huhusisha mitindo fulani ya ki-usemi na misimbo fulani ambayo imesaidia katika uashiriaji wa kazi za baadaye.

Mawazo ya Kristeva yamewekewa msingi na mawazo ya Bakhtin. Kwa hakika Kristeva ndiye aliyemfanya Bakhtin afahamike kwa kuyaendeleza mawazo yake. Dhana iliyomwathiri Kristeva katika uhakiki wa Bakhtin ni ile ya 'usemezano' au 'usemezo' ambapo katika matini moja kunakuwepo na maana nyingi. Hivi ni kumaanisha kwamba matini za kifasihi huakisiana kwa namna moja au nyingine kiasi kwamba zinachangizana katika uashiriaji wa maana. Bakhtin aliamini kuwa, mwandishi anapoanza kuandika hujiingiza kwenye usemezano wa aina fulani na mwandishi aliyemtangulia. Kwa hivyo, panakuwako na sauti zinazojibizana. Aidha Julia Kristeva ana maoni kufu na haya kwani katika Kristeva (1980) anasema:

> Matini ni kama jira mbili. Jira ya mlalo ambayo inaunganisha mwandishi na msomaji wa matini na jira ya wima inayounganisha matini na matini zingine. Jira hizi mbili nazo, zinaunganishwa na ishara moja zinazotumika kwa kuwa kila matini na kila usomaji unategemea ishara zilizokuwako awali. (Uk. 66) (Tafsiri yetu).

Bakhtin anaendelea kusema kuwa maana ya matini za kifasihi hazitokani na sifa za kiisimu, kiuchumi au kijamii pekee. Kwake matini ya kifasihi ni uwanja fulani na kwenye uwanja huo kuna mwingiliano wa sauti anuwai. Kuhusu semi Bakhtin (1990) anasema kuwa semi zote kimaumbile ni za kisemezano. Hii ina maana kuwa kila usemi ni jibu la kitu kingine na hutarajiwa kujibiwa.

Mtaalamu mwingine ambaye amechangia katika uchanganuzi wa nadharia hii ni Ronald Barthes. Kwa mujibu wa Barthes (katika Allen, 2002), maana ya kazi ya kifasihi hahifadhiwi na kazi yenyewe bali kazi hutoa muktadha ambapo mifumo mingi huungana. Maoni yake ni sahihi kwa kuwa maana tofauti zinaweza kuibuliwa kutokana na kazi moja. Anadai kuwa kazi ya kifasihi inaweza kueleweka kwa kuilinganisha na kazi nyingine. Msomaji hastahili kujifunga katika matini pekee ila anafaa kuilewa kwa mujibu

wa uhusiano wa kazi na miundo ya kiisimu. Katika kuendeleza umantiki wa nadharia hii, Bakhtin (1986:93) katika insha moja anasema:

> Msemaji si Adamu katika biblia, anayehusika tu na bikira na vitu visivyopewa majina na kuvipa majina kwa mara ya kwanza. Ukweli ni kuwa kila kauli au usemi hujibu au hurejelea kwa njia moja au nyingine usemi mwingine uliotangulia. (Tafsiri yetu).

Wataalamu wengine ambao wamechangia katika uchanganuzi wa nadharia hii ni Plottel na Charney (1978). Hawa wanasema kuwa matini ya kisanaa si zao la mwandishi mmoja bali ni zao la jinsi matini hiyo huhusiana na matini nyingine na miundo ya lugha yenyewe. Dhana ya mwingilianomatini inasisitiza kuwa matini zote za kisanaa zaweza kuchukuliwa kama matini moja kuu ambapo hujibizana; kila moja ikisemezana na nyingine kwenye usemezano uliotanuliwa. Aidha matini zote huhusiana kwa njia moja au nyingine na vilevile matini zenyewe hutegemeana ili kuzalisha maana.

Kwa jumla, maoni ya Wamitila (2002:137) yanatutamatishia msingi wa nadharia yetu. Kwake sifa ya mwingilianomatini inajitokeza kwa njia kadha kama mwangwi wa dhamira au maudhui. Kazi fulani inaweza kuakisi nyingine kimaudhui kwa kuongelea dhamira au maudhui yale yale. Katika utafiti wetu tumechunguza iwapo tamthilia hizi mbili zinaongeleana, zinahusiana au kutegemeana. Tumejikita katika mkabala wa kiuhakiki unaohusishwa na Julia Kristeva na wataalamu wengine wanoafikiana naye kuwa hakuna matini yoyote ya kifasihi inayoweza kuangaliwa kivyake. Utafiti huu umetalii na kuzihakiki tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* na kudhihirisha kuwa matini za kifasihi huingiliana.

Kutokana na maelezo ya nadharia ya Mwingilianomatini ni bayana kuwa mihimili yake inaweza kusemekana kuwa:

i. Hamna matini yoyote ile ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake au kujitegemea.

ii. Matini yoyote ile ni mabadiliko ya mpangilio wa matini nyingi tangulizi.

iii. Kazi za kifasihi huundwa kutokana na mifumo ya kanuni na tamaduni mbalimbali zilizowekwa na kazi tangulizi za kifasihi ambapo taswira za maisha ya kawaida na uhusiano wa kimaana huunganishwa na kubadilishwa.

iv. Matini moja hufafanua usomekaji wa mkusanyiko wa matini zote za kongoo moja, ambapo matini tangulizi hufyonza na kujibiwa na matini mpya.

v. Kila usomaji wa matini huwa ni kijalizo cha matini tangulizi na hivyo basi huigeuza kwa kiwango. Kwa jinsi hii kauli inayonukuliwa hubadili na kuelezea upya kauli asilia kwa kuiambatanisha na muktadha mwingine wa kiisimu na kijamii.

### 1.8 Yaliyoandikwa kuhusu mada

Kufikia sasa na kwa mujibu wa utafiti wetu, yaliyoandikwa kuhusiana na somo hili si mengi. Hata hivyo, kuna baadhi ya wahakiki au waandishi ambao wameliandikia somo hili kwa kina ilhali wengine wameligusia tu.

Mugambi (1982), ametafitia tamthilia zilizoandikwa nchini Kenya kati ya mwaka 1956 hadi 1982. Anaeleza kuhusu maendeleo ya tamthilia kulingana na maudhui yanayojitokeza. Kwake yeye, wanathamthilia wa kwanza nchini Kenya wanaendeleza mitazamo ya kikoloni katika utunzi wao kama vile Hyslop (1957), Kuria (1957) na Ngugi (1961). Kizazi cha pili ni cha waandishi ambao wamekengeuka kutokana na jamii zao kama vile Osodo (1979) na Kitsao (1980). Kwa maoni yake, watunzi wanaotumia sanaa kama chombo cha ukombozi ni kama vile Ngugi wa Thiong’o na Mugo (1978) na Said (1980). Utafiti wake ulitusaidia kuelewa tamthilia za Kikenya au watunzi wa Kikenya ambao huenda waliwaathiri au waliathirika na waandishi tunaowachunguza. Aidha tumeelewa kuna maudhui ambayo yanaingiliana kati ya kazi za waandishi hawa tunaowachunguza na wale ambao Mugambi (1982) aliwatafiti.

Huku akieleza historia ya tamthilia nchini Tanzania, Mlama (1983) anasema tamthilia ilitungwa kwa minajili ya kutumiwa na serikali ya kikoloni kuwasisimua wahudumu wa serikali na kumsimanga mwafrika kwani ilimsawiri mwafrika kama kiumbe duni. Baada ya uhuru, futuhi zilitungwa za kuwakashifu waafrika walioiga mienendo ya wazungu bila kufikiria. Baadaye kidogo, ndipo watunzi wa tamthilia walianza kuambatanisha tamthilia na hali ya kiuchumi ya kijamii. Mawazo yake yalitufaa sana katika kuchunguza ikiwa tamthilia ya Kiswahili inakashifu wale watu wanaofuata mienendo ya wazungu kikasuku kupitia sauti mbalimbali za kijamii au la.

Wamitila (1997) katika makala yake kuhusu kazi za Kezilahabi, anahakiki motifu za dunia kama mahali pabaya na maisha kutokuwa na maana. Anachunguza namna kazi za

Kezilahabi zinadhihirisha kuwa dunia ni mbaya na inastahili kutazamwa kama mahali pabaya pa kuishi. Vilevile, anachunguza jinsi kazi za mwandishi huyo zinavyodhihirisha kuwa maisha ni mafupi na kwamba binadamu anapaswa kufurahia wakati huu ambao yu hai. Wamitila anajikita katika kazi za kinathari za Euphrase Kezilahabi, *Rosa Mistika* (1971), *Kichwa Maji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo*(1975), *Gamba la Nyoka* (1978), *Nagona* (1990) na *Mzingile* (1990). Japo mwandishi hakushughulikia swala la mwingilianomatini katika kazi hizi, makala yake yalitufaa kwa kuwa yanaangazia maisha ya binadamu katika ulimwengu.

Wafula (1999) anahakiki tamthilia kumi na nne za Kiswahili. Anachukulia tamthilia iliyoandikwa kama kazi nyingine yoyote ya kifasihi iliyokamilika na kuihukumu kwa misingi ya kifasihi. Anaonyesha maudhui muhimu yanayoshughulikiwa na waandishi wa tamthilia za Kiswahili na kuonyesha jinsi tamthilia za Kiswahili zilivyo na ukwasi mkubwa kimtindo. Kazi hii imetufaa kwa kututolea mwanga zaidi kuhusu tamthilia mbalimbali za Kiswahili na kuzielewa kwa undani. Aidha imetufaa kwani inaeleza historia fupi ya uandishi na uhakiki wa tamthilia. Hata hivyo, kazi yetu ni tofauti kwani tasnifu yetu imezingatia nadharia ya Mwingilianomatini ili kuweza kuchunguza vipengele anuwai katika mwanda wa kimwingiliano.

Nzuki (2003) katika tasnifu yake anashughulikia mwingiliano wa fani na maudhui katika diwani za *Mchezo wa Karata* (1997) na *Bara Jingine* (2001). Aliongozwa na nadharia ya Sosholojia na ameonyesha umuhimu wa vipengele vya kifani pamoja na athari za kimazingira katika kujenga fahiwa katika kazi za kifasihi. Mambo mawili makuu yanajitokeza katika utafiti wake. Kwanza, zote zinafuata mkondo wa ushairi huru na pili, mtunzi amezua mbinu mpya za kuandika mashairi huru ya sitiari za michoro kwa kuonyesha kuwa kinachoonekana katika michoro hakiwezi kutenganishwa na yale yanayoelezwa kupitia maneno ya mtunzi.

Ochoki (2005) katika tasnifu yake anahakiki riwaya mbili za Kezilahabi; *Nagona* na *Mzingile*. Anazilinganisha na kuzitofautisha na kazi zake za kinathari za awali *Rosa Mistika* (1971), *Kichwa Maji* (1974) na *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975). Hali kadhalika anachunguza maendeleo ya kazi zake hasa upande wa maudhui na baadhi ya vipengele vya fani kama jazanda na sitiari. Aidha anadhihirisha jinsi ambavyo matini za kifasihi huingiliana hasa upande wa kutumia mbinu za fasihi simulizi na fasihi andishi kwa kuzingatia visasili katika riwaya za *Pedro Paramo* na *Babu Alipofufuka*. Kwa ufupi kazi

ya Ochoki inatoa mchango mkubwa katika kuzieleza kazi hizi vyema ingawa ina udhaifu wa kutodhihirisha waziwazi kama kuna mwingilianomatini kati ya *Nagona na Mzingile* zikilinganishwa na *Pedro Paramo*. Analoonyesha wazi ni kuwa *Nagona* na *Mzingile* ni riwaya moja.

Njoroge (2007) katika tasnifu yake anahakiki riwaya mbili za waandishi wawili, Euphrase Kezilahabi, *Rosa Mistika* (1971) na Said A. Mohamed, *Tata za Asumini (*1990) Nadharia ambayo imemwongoza ni ya Mwingilianomatini. Aidha ametalii vipengele anuwai katika mwanda wa kimwingilianomatini kama vile ploti, wahusika, mandhari na maudhui. Isitoshe, anaonyesha namna riwaya hizi zinavyohitilafiana kwa kiasi tu katika kipengele cha ploti na wahusika. Hata hivyo, Njoroge hakushughulikia vipengele vyote katika mwanda wa kimwingilianomatini. Kwa Ufupi, kazi ya Njoroge imetoa mchango mkubwa katika kuzieleza kazi hizi. Tumetumia kazi hii kama msingi wa kutuwezesha kuhakiki vipengele anuwai vya kifani katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu* wa *Serikali* na *Mstahiki Meya*. Vipengele vya kimwingilianomatini ambavyo tumeshughulikia katika utafiti wetu ni ploti, wahusika, mandhari na maudhui.

Bakari (2011) anatafiti dhana ya usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alipofufuka* (2001), *Bina-damu !* (2002) na mkusanyiko wa hadithi fupi wa *Sadiki Ukipenda* (2002). Katika utafiti huu anabainisha vipengele mbalimbali vya kiuhalisiajabu na kuonyesha jinsi watunzi wa riwaya hizi wanavyotumia uhalisiajabu ili kuonyesha matatizo yanayoibuka katika ulimwengu wa sasa. Mtafiti huyu anaangazia maudhui katika riwaya mbili na hadithi fupi. Utafiti wake ulitusaidia kuelewa mawazo mbalimbali yanayoibuka katika kazi za kifasihi.

### 1.9 Mbinu za utafiti

Utafiti wetu umehusu usomaji wa kina maktabani. Hii ni kwa sababu huu ni utafiti wa kifasihi. Data ya kimsingi katika utafiti wetu imetolewa kutoka tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya*. Mbali na tamthilia hizi mbili, kazi nyingine za kifasihi zenye mielekeo ya kimwingilianomatini zimesomwa ili kutuwezesha kupata mwanga zaidi. Vilevile makala maridhawa kuhusu tamthilia za Kiswahili pamoja na uhakiki wake yalisomwa ili kutusaidia kuelewa utanzu wa tamthilia ipasavyo. Aidha tumesoma baadhi ya tamthilia za Kiswahili zikiwemo : *Kilio cha Haki* (1981), *Kifo Kisimani* (2004) na *Upepo wa Mvua* (2013) kati ya nyingine na zimetupa ufahamu zaidi kuhusu maswala ya uongozi na maadili sawa na tamthilia zetu teule. Mifano ya mambo

yanayoingiliana imetolewa ili kuweza kubainisha kuwa maandishi haya yanaingiliana au la. Hatimaye tumetoa mahitimisho na mapendekezo ya utafiti.

# SURA YA PILI

## MWANDA WA KI- MWINGILIANO KATIKA FASIHI

### 2.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumehakiki na kutathmini vipengele anuwai vya kifasihi katika mwanda wa kimwingilianomatini. Kwa mujibu wa Wamitila (2003: 114) mwanda ni dhana inayotumiwa kuelezea upana wa kimahusiko wa kazi ya kifasihi. Upana huu unaweza kuwa wa kimazingira au mandhari, undani wa wahusika, swala la wakati na kadhalika. Kama tulivyosema katika sura ya kwanza, nadharia ya Mwingilianomatini huchukulia kuwa kazi ya kifasihi inahusiana na kazi nyingine na kwamba kazi yoyote ile huwa na maana kwa sababu mambo fulani yanayohusiana nayo yamekwisha kuandikwa tayari. Mwingiliano ni ule uingiliano na uhusiano wa mitindo ya kiuashiriaji.

Kwa jumla, matini za kifasihi huakisiana. Akisio hilo linaweza kutokea kwenye mtiririko wa vitushi, usawiri wa wahusika, uelezaji wa mandhari, matumizi ya taswira, dhamira, maudhui na vilevile katika mitindo ya kisimulizi. Hata hivyo, matini haziingiliani katika vipengele vyote. Baadhi ya matini huingiliana katika kipengele kimoja ilhali nyingine huingiliana katika vipengele zaidi ya kimoja. Kwa mujibu wa utafiti wetu, tutajikita kudhihirisha mwingiliano katika msuko, wahusika, uelezaji na ujenzi wa mandhari na maudhui. Tumezifafanua dhana hizi kama msingi wa kuhakiki tamthilia hizi mbili kimwingilianomatini.

### 2.2 Vipengele vya mwanda wa kimwingilianomatini katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya.*

### 2.3 Msuko

Msuko ni kipengele mojawapo katika mwanda wa kimwingilianomatini. Waandishi tofauti huingiliana kimsuko. Yaani matini zao huingiliana kwa mujibu wa mpangilio wa vitushi kiusababishi. Msuko ni mtiririko wa vitushi katika kazi ya fasihi. Katika msuko, msanii hutanguliza na kitendo cha kwanza na kuonyesha vile vitendo hufuatana na kuathiriana hadi kufikia mwisho wa kazi yake. Msokile (1993:35) alisema msuko ni mfululizo wa matukio yanayosimuliwa katika hadithi. Mhakiki anapofanya uhakiki wake anajaribu kuchunguza jinsi mwandishi alivyounda au kufua na kuunganisha matukio yake, vitendo na mawazo. Kwa mujibu wa Wamitila (2002:6) msuko ni mpangilio wa

matukio yanayopatikana katika kazi ya kifasihi kwa kutegemea uhusiano wake kiusababishi yaani, tukio fulani linasababishwa na nini? Msuko ni kipengele muhimu katika hadithi yoyote ile. Uchunguzi wowote wa msuko unajihusisha na kile kinachoweza kuitwa visababishi. Msuko unahusu kujiuliza swali la kwa nini tukio fulani limetangulia jingine. Wamitila (2003) ameanisha misuko mbalimbali: msuko kinzani, msuko msago, msuko mkuu, msuko kioo na msuko rudufu.

### 2.3.1 Msuko mkuu

Msuko huu unahusu hadithi kuu katika kazi ya kifasihi. Msuko mkuu hupatikana pale ambapo kazi ya kifasihi ina hadithi kadha ambazo kila moja ya hadithi hizo inatambulika. Kimsingi, msuko mkuu huhusisha matendo na maelezo kuhusu mhusika mkuu katika kazi ya kifasihi.

### 2.3.2 Msuko kinzani

Hii ni ploti inayoeleza matukio ambayo yanakusudia kufikia lengo tofauti na lile la msuko mkuu. Hoja hii ina maana kuwa msuko wa aina hii huhusishwa na mhusika anayepingana na mhusika mkuu. Mhusika wa aina hii atatenda matendo yanayoonyesha kupinga au kuakisi matendo au mwelekeo unaochukuliwa na mhusika mkuu.

### 2.3.3 Msuko msago

Hutumiwa kueleza matukio yanayofuatana kwa njia ya moja kwa moja bila ya kuwa na matumizi ya mbinu rejeshi. Wamitila (2003:143) anaeleza kuwa matukio hufuatana kwa njia ya A-B-C-D na kadhalika. Waandishi wengine huurejelea msuko wa aina hii kama msuko sahili. Misuko yote ya tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* ni sahili.

### 2.3.4 Msuko kioo

Msuko kioo ni aina ya msuko ambao unaenda nyuma na mbele. Msuko wa aina hii huhusisha mbinu rejeshi kwa wingi. Msuko huu pia huitwa msuko changamano. Msuko huu hautumiwi sana katika utanzu wa tamthilia.

### 2.3.5 Msuko rudufu

Msuko rudufu ni msuko ambao unahusisha zaidi ya msuko mmoja katika kazi ya kifasihi. Misuko inayopatikana katika kazi ya aina hiyo inafaa kuwa na nafasi sawa. Yaani hadithi mbalimbali zinazopatikana katika kazi hiyo zinaweza kujisimamia na kila

moja ikatambuliwa waziwazi.

Katika tasnifu yetu, tumehakiki namna tamthilia hizi mbili zinavyoingiliana kimsuko. Aidha, tumeonyesha jinsi matukio yanavyofuatana kiusababishi katika kazi zote na kutathmini kiwango cha mwingiliano wazo.

## 2.4 Wahusika

Wahusika ni kipengele kingine katika mwanda wa kimwingilianomatini. Wahusika ni viumbe wanaotumiwa na msanii kuwasilisha mawazo yake. Viumbe hawa wanaweza kuwa wanyama au binadamu. Kulingana na Njogu na Chimerah (1999:45), wahusika ni sehemu ya fani na ni viumbe wa sanaa wanaobuniwa kutokana na mazingira ya msanii. Mazingira haya huweza kuwa ya kijiografia, kihistoria, kijamii, kitamaduni au ya kisiasa. Wahusika hujadiliwa kwa namna wanavyoingiliana na maudhui na hili hujitokeza kutokana na maneno, tabia na matendo yao, yaani kulingana na hulka yao. Wahusika wa aina yoyote wawe watu au viumbe hurejelea na huakisi sifa na tabia za binadamu katika jamii. Wamitila (2003: 199) anasema wahusika ni viumbe au watendaji wanaopatikana katika kazi ya kifasihi. Viumbe hawa ni kama nguzo kuu ya dhamira na maudhui. Hii ni kwa sababu kila tendo lazima liwe na mtendaji. Wahusika wanafanana kwa kiasi kikubwa na binadamu katika maisha ya kawaida lakini sio lazima wadhibitiwe na kanuni zote za binadamu halisi. Wahusika hutumiwa kuiwakilisha hali halisi ya maisha ya binadamu katika jamii fulani. Wamitila anaendelea kusema kuwa wahusika wa tamthilia wanadhihirishwa au kuelezwa haraka kwa njia waziwazi na zisizotatanisha.

Kulingana na Wamitila (2008:368), wahusika ni nyenzo kuu ya kifasihi kwa sababu wao ndio jira ya matukio na matendo yanayopatikana katika kazi ya kifasihi inayohusika. Mtazamo wa dhana ya wahusika hutofautiana kutegemea mkabala anaochukua mhakiki wa nadharia ya fasihi inayohusika. Kwa hivyo, mhusika ni mtendaji katika kazi ya kifasihi na huwa kielelezo cha viumbe wanaopatikana ulimwenguni ingawa si lazima sifa zote za mhusika zifungamane moja kwa moja na za wanadamu.

Katika tasnifu yetu, tumejikita katika kudhihirisha jinsi wahusika wanavyoingiliana katika kazi teule. Swala la wahusika kuingiliana limekuwepo na litakuwepo. Waandishi tofautitofauti wanaweza kumsawiri mhusika au kuwasawiri baadhi ya wahusika kwa njia zinazofanana mathalani wahusika wanaweza kuwa na hulka sawa, asili moja na aidha majina yanayolandana. Ingawa waandishi tofauti wanaweza kuwapa wahusika majina

tofauti, si ajabu kuona kuwa wahusika wao hao wana uhusiano kisifa, katika asili na aidha mwono-ulimwengu.

Mwingiliano wa kiwahusika unajitokeza katika hadithi au kazi nyingi za kifasihi. Mathalani, kuna mwingilianomatini katika usawiri wa wahusika kati ya *Kifo Kisimani* na *Usaliti Mjini*. Wahusika Bokono na Mwelusi katika *Kifo Kisimani* wanaingiliana kwa kiwango kikubwa na wahusika Tumbo na Adika katika *Usaliti Mjini*. Vilevile, Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya wanashabihiana si haba. Aidha tunaona mwingilianomatini katika usawiri wa wahusika katika *Upepo wa Mvua* na *Wingu la Kupita*. Wahusika hawa ni Kidani katika *Upepo wa Mvua* na Jaribosi katika *Wingu la Kupita*. Swala la waandishi tofauti kuwasawiri wahusika wao kwa njia zinazolandana tumelifafanua kwa mapana na marefu katika sura ya nne.

### 2.4.1 Usawiri wa wahusika

Wamitila (2003: 312) anasema yafuatayo kuhusu dhana ya kuwasawiri wahusika:

> Hii ni dhana inayotumiwa kuelezea jinsi wahusika wa kifasihi walivyochorwa au kuwasilishwa na msanii au mtunzi wa kazi fulani. Usawiri wa wahusika huhusisha majina yao, lugha wanazopewa na matumizi yao ya kifasihi.

Mwandishi anaweza kutumia njia kadha na tofauti katika kuwasawiri wahusika wake. Msanii ana uhuru sio tu wa kuwatumia wahusika wa aina fulani, bali wa kuteua namna ya kuwawasilisha wahusika wenyewe.

#### 2.4.2.1 Mbinu za kuwasawiri wahusika

Kuna mbinu kadha ambazo waandishi huweza kutumia katika kuwasawiri wahusika. Wahusika huweza kuwasilishwa kwa njia dhahiri au isiyokuwa dhahiri, kudhihirishwa na kuendelezwa kwa njia tofauti, kuanzia za kijuujuu hadi za undani au kina hadi kwa undani wa kisaikolojia. Zifuatazo ni baadhi ya mbinu za kijumla ambazo hutumiwa kuwasawiri wahusika katika kazi za kifasihi.

#### 2.4.2.2 Maelezo au maneno ya wahusika wengine

Njia hii huhusu maelezo ambayo yanatolewa na mhusika kuhusu mwingine au wengine. Mara nyingi, mtindo huu hutuelekeza kimsingi kwenye mkabala wa mhusika

anayehusika. Hata hivyo, maelezo ya mhusika mmoja kumhusu mwingine huenda yasitegemewe hasa kutokana na uwezekano wa maelezo hayo kuathiriwa kwa kiasi kikubwa na mtazamo wa mhusika binafsi. (Wamitila 2002:23)

#### 2.4.2.3 Mbinu ya matendo au matumizi ya mazungumzo

Pia huitwa 'Mbinu ya Kidrama'. Katika mbinu hii, maneno yanayosemwa na wahusika baina yao huwa ni msingi mkubwa wa kuwakuza na kuwaendeleza wao hao wahusika. Mtunzi huwakuza kwa kuonyesha wahusika wakitenda matendo au kuzungumza huku akiwaacha wasomaji wawaone na kuzichanganua tabia zao kutokana na matendo au mazungumzo yao. Mazungumzo huchukuliwa kama njia ya kuendeleza mgogoro (tendo) ulioko katika kazi ya kifasihi au dhamira na maudhui. Hutekeleza kazi ya kumsawiri mhusika. Matendo ya wahusika yanaweza kutuelekeza katika kuelewa tabia, imani, mategemeo au matumaini, hisia zao, kero zao, ndoto zao au hata udhaifu wao (Njogu na Chimerah (1999: 46) na Wamitila (2008: 376).

#### 2.4.2.4 Mbinu ya majazi

Katika tamthilia kama ilivyo katika baadhi ya tanzu zingine za kifasihi, majina huwa ni msingi muhimu wa uhusika. Katika mbinu hii, baadhi ya waandishi hutumia majina ambayo yanafumbata tabia, sifa au matendo ya wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi zinazohusika. Kwa njia hii, msomaji huweza kuifahamu tabia na wasifu wa mhusika kwa urahisi zaidi. Vilevile, mtunzi huweza kuchimuza mtazamo na mwono wake kuwahusu wahusika fulani na hata mwelekeo wa hadithi nzima. Hata hivyo, kuna udhaifu kwa kuwa msomaji hashirikishwi katika uamuzi wa wasifu wa mhusika; hulazimika tu kuridhika na maoni ya mwandishi. Mara nyingi, njia hii ya kuwasawiri wahusika huhusisha matumizi ya kinaya au kejeli na mihusianisho na ishara. (Wamitila (2008:170, 378).

Mifano ya wahusika waliopewa majina ya majazi ni wengi katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya*. Kuna Mkuu wa Wilaya, Mratibu wa Elimu, Bw. Huruma, Bw. Hakimu, Bw. Posta, Mstahiki Meya, Siki, Waridi, Bili na wengineo.

#### 2.4.2.5 Maelezo ya msimulizi au mwandishi

Katika mbinu hii, msimulizi anaweza kueleza wasifu wa mhusika, msukumo wa matendo yake, mazingira yake, tabia na amali zake ili msomaji auone mtazamo huo na labda hata

akubaliane naye. Kwa kiasi kikubwa mhusika mwenyewe anakuwa kiumbe asiyekuwa na uwezo wa kuathiri mtazamo huo unaomwangalia kwa nje. Njia hii hujulikana kama 'uhusika wa kimuhtasari' kutokana na ile hali kuwa mwandishi anatoa muhtasari wa mhusika fulani kwa maneno au sentensi kadha. (Wamitila 2008:171, 376).

#### 2.4.2.6 Mbinu ya mwingilianomatini

Matini za kifasihi huhusiana na kuingiliana kwa njia tofauti. Kuingiliana huko kunaweza kutokeza katika viwango tofauti vikiwemo kiwango cha hadithi inayohusika, dhamira, ishara au sitiari na kiwango cha usawiri na uendelezaji wa wahusika. Kazi za kifasihi ambazo zimekitwa katika matumizi ya simulizi-kuu za jamii fulani au za utamaduni wa kimagharibi, zinaonyesha waziwazi sifa hii katika usawiri wa wahusika (Wamitila 2008:380-381). Waandishi Gogol na Arege wamewasawiri wahusika wao kwa njia zinazolandana. Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya, Bw. Hakimu na Diwani I, Bw. Huruma na Diwani II, Yosif na Dida, Ghlestakovu na Bili, Askari, Wafanyibiashara na Wafanyikazi wanadhihirisha kiwango cha juu cha mwingiliano.

Mbinu hizi ni za kijumla tu ambazo hutumiwa katika fasihi na waandishi wote wanapoandika kazi zao.

### 2.5 Dhamira na maudhui

Hizi ni dhana muhimu sana katika uhakiki wa kimwingilianomatini na uhakiki wa fasihi kwa jumla. Katika matumizi ya kawaida, neno dhamira hutumiwa kurejelea lengo kuu la mwandishi wa kazi fulani. Mwandishi anapoanza kuandika tamthilia au kazi yake, huwa na lengo fulani linalomsukuma kuiandika kazi hiyo.

Kimani na Chimerah (1999:23) wana maoni kuwa dhamira ni lengo au shabaha ya kazi ya fasihi. Maoni haya yanashadidiwa na Wamitila (2002:53-54) anayesema kwamba dhamira hutumiwa kurejelea swala fulani au ujumbe au lengo la kazi hiyo. Dhamira ni ile jumla ya maana anayoivumbua mwandishi aandikapo na jumla ya maana anayoitambua msomaji katika usomaji wake. Tunaweza kuivumbua maana ya kazi fulani kwa kuisoma kazi hiyo kwa kina na makini, huku tukiuelewa na kuung'amua uhusiano wa visehemu mbalimbali pamoja na jinsi visehemu hivyo vinavyohusiana na kazi nzima na kuvyaza kitu kimoja. Dhamira kwa upande wake haiyahusishi majibu bali huzua maswali. Dhamira pia huingiliana na vipengele vingine vya kazi ya kifasihi ili kuunda kitu kimoja. Vipengele hivi ni pamoja na dhamira na wahusika, msuko, uhamasishaji, mandhari,

mtindo, thamani, toni na kadhalika. Dhamira hizo huweza kuwa za aina mbalimbali kwa mfano, kilio cha wanyonge na ukombozi katika *Kilio cha Haki* ya Mazrui, uongozi mbaya na umaskini katika *Wingu la Kupita* ya Wamitila au ukoloni na ukoloni mamboleo katika *Mashetani* ya Euphrase kezilahabi.

Kwa upande mwingine, tumehakiki jinsi tamthilia hizi zinavyoingiliana na kuchangizana kimaudhui. Kwa mujibu wa Kimani na Chimerah 1999:21 maudhui ni ujumbe wa jumla kuhusu matukio, kitu, wahusika au hali ya maisha kama yanavyojitokeza katika kazi au fasihi, iwe riwaya, tamthilia, shairi au wimbo. Maudhui ni sehemu ya maana na huingiliana na mada. Ni katika maingiliano baina ya mada na maudhui ambapo ukweli uliokusudiwa na mwandishi hujitokeza. Naye Wamitila (2002; 137) anasema kuwa, kazi fulani inaweza kuiakisi nyingine kimaudhui, yaani kwa kuiongelea dhamira au maudhui yale yale. Si ajabu kupata kazi mbili ambazo zinazungumzia maswala sawa. Kwa mfano tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Wilaya* na *Mstahiki Meya* zinagusia maswala ya ufisadi, ukosefu wa uwajibikaji, usaliti, dhuluma, tamaa, ubadhirifu na unafiki. Jambo hilo linashadidia kauli kuwa, hakuna kazi ya kifasihi inayoweza kuangaliwa kivyake.

## 2.6 Mandhari

Mbali na ploti, wahusika, dhamira na maudhui, waandishi wa kazi za kifasihi wanaweza kuingiliana kimandhari. Matendo yoyote ambayo hutokea katika kazi za kifasihi hufanyika mahali fulani na wakati maalumu. Hiki ndicho kinachoelezwa kama mandhari. Kwa hivyo, mandhari ni elementi ambayo hufichua ni wapi ambapo matukio fulani yanafanyika. Njogu na Chimerah (1999: 46) wanasema mandhari ni mahali au makazi maalumu yaliyojengwa na mtunzi; na mnamotukia matukio mbalimbali ya kifasihi. Mandhari ni mazingira ya wahusika pamoja na matukio na inahusu mahali wanamokaa wahusika na kuingiliana; mazingira ya kijamii na kiuchumi ya wahusika hao; na nafasi zao za kitabaka. Maoni haya yanashadidiwa na Wamitila (2003:210) anayesema kwamba, mandhari hutumiwa kuelezea sehemu ambako tendo fulani hutendeka. Neno hili huweza kutumiwa kwa mapana kuelezea pia mazingira ya kisaikolojia ya tendo fulani. Mandhari huweza kurejelea yale mazingira ya jukwaani na hata wakati wenyewe. Mtunzi anaweza kutusawiria mandhari ya kijiografia ambayo ni vitu kama vile mito, milima na misitu. Mazingira aidha yaweza kuwa ya kijamii kama vile nyumbani, ofisini, shuleni, hospitalini na kadhalika.

Katika maelezo haya, Wamitila anafafanua upana wa mandhari. Anasema kwamba,

mandhari si mazingira tu bali hurejelea maswala mengi yakiwemo itikadi, mila, desturi, jamii na elimu. Hivyo, ina maana kuwa mandhari yanaweza kuhamishwa katika mazingira tofauti kulingana na muktadha. (Wamitila 2002:27).

Mandhari huchangia katika kueleza mambo mengi kuhusu sifa na tabia za wahusika, hali yao na huweza kuwa mihimili mikuu ya kuyaendeleza maudhui ya kazi ya kifasihi. Aidha matendo ya wahusika huchochewa na mandhari na mazingira yao. Mazingira anamojikuta mhusika yanaathiri kwa kiasi kikubwa wasifu wake kama mhusika. Mara nyingi, wasomaji hupenda kuona mandhari yanayoweza kutambulika lakini hili haliwezekani katika kazi ambazo haziandikwi katika misingi ya uhalisia.

Kutokana na maelezo ya wataalamu hawa, mandhari ni kama kipengele cha kudhibiti wahusika na ni muhimu katika kuchanganua kazi za kifasihi. Kwa hivyo, mandhari yana dhima au majukumu mbalimbali katika kazi za kifasihi; na ambayo hutofautiana kulingana na malengo ya msanii anayehusika. Wanasema kuwa kufahamu mandhari husaidia wasomaji kuelewa hisia, imani, tabia na maumbile ya wahusika. Pili, mandhari yanatupa mwelekeo kuhusu maudhui. Swala hili la waandishi kuchangizana na kuingiliana kimazingira katika utunzi wao tumelishughulikia katika sura ya tatu.

**2.7 Vipengele vingine vya kimwingilianomatini**

Kazi za kifasihi kadhalika huakisiana katika matumizi ya taswira na aidha mtindo wa kisimulizi. Kazi anuwai zaweza kutumia taswira moja katika kuendeleza maudhui yake. Mfano mwafaka ni matumizi ya taswira ya safari na kifo katika riwaya za kezilahabi *Nagona* na *Mzingile*. Kazi tofauti huweza kuingiliana katika mtindo wa kisimulizi. Riwaya ya Ruflo ya *Pedro Paramo* na *Nagona* na *Mzingile* za Kezilahabi zinaingiliana katika mtindo wa kisimulizi. Taswira ya safari na ya kifo zimetumika katika kuendeleza maudhui ya kazi hizi.

Hata hivyo, kuna njia bainifu au wazi za mwingilianomatini. Hizi ni kama vile unukuzi au udondoaji. Baadhi ya waandishi wa tamthilia hupendelea kutanguliza tamthilia zao kwa ushairi au dondoo tangulizi. Mashairi haya aghalabu hudondolewa kutoka diwani za mashairi. Mfano ni kuwepo kwa dondoo tangulizi katika tamthilia ya *Amezidi* ya Said Ahmed Mohamed kutoka tamthilia ya *Kilio cha Haki* ya Alamin Mazrui. Si ajabu pia kuona waandishi fulani wakizinukuu kazi za waandishi wengine moja kwa moja katika kazi zao.

Tumevifafanua vipengele hivi vya kimwingilianomatini kwa kirefu katika sura ya tatu, nne na ya tano.

### 2.8 Hitimisho

Katika sura hii, tumetanguliza kwa kufafanua vipengele anuwai katika mwanda wa kimwingilianomatini. Tumefafanua kipengele cha msuko na aina za misuko.

Vilevile, tumeshughulikia kipengele cha wahusika na usawiri wa wahusika katika kazi za kifasihi. Kisha tukafafanua mbinu ambazo watunzi tofauti huzitumia katika kuwasawiri wahusika katika kazi zao za kifasihi. Tumeshadidia kauli kuwa kazi za kifasihi huingiliana na kuchangizana kiwahusika. Hivi tumedhihirisha kwa mifano kutoka baadhi ya kazi za kifasihi. Hata hivyo, swala hili la mwingiliano wa kiwahusika katika kazi za Kiswahili tumeliendeleza katika sura ya nne.

Aidha, tumefafanua dhamira na maudhui kama vipengele vya kimwingiliano. Kazi za kifasihi huingiliana kidhamira na kimaudhui. Tumetoa mifano kadha ya dhamira ambazo huweza kujitokeza katika kazi za kifasihi.

Hali kadhalika, tumefafanua kipengele cha mandhari kama mazingira ya utendaji au usimulizi. Tumeona kuwa waandishi tofauti wanaweza kutusawiria mandhari sawa katika kazi zao tofauti. Mazingira haya yanaweza kuwa ya kijiografia au ya kijamii. Uteuzi wa mandhari mwafaka huipa kazi fulani tapo la uhalisia au ushabihi kweli. Katika sura ya nne, tumelishughulikia swala la kimwingilianomatini huku tukiangazia kipengele cha mandhari.

Hata hivyo, katika sura hii hatukuweza kufafanua vipengele hivi vya kimwingiliano vya kutosha. Katika sura ya tatu, nne, na tano tumehakiki jinsi tamthilia hizi zinavyoingiliana na kuchangizana kwa mujibu wa kipengele hivi na kama inavyodaiwa na wananadharia wa mwingilianomatini.

# SURA YA TATU

# MSUKO NA MWINGILIANOMATINI

## 3.1 Utangulizi

Sura ya pili imeshughulikia vipengele mbalimbali katika mwanda wa kimwingilianomatini. Katika sura hii, tumehakiki kipengele cha msuko na kuonyesha namna tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na ile ya *Mstahiki Meya* zinaingiliana kimsuko. Hapa chini tumehakiki msuko katika tamthilia hizi na kudhihirisha jinsi kazi hizi zinavyoingiliana na kuchangizana.

## 3.2 Msuko katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*

Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* inazungumzia uongozi wa Mkuu wa Wilaya. Kiongozi huyu amepatiwa mamlaka ya kusimamia polisi na usalama wa mji. Anasaidiana na Bw. Huruma, Bw. Hakimu na Mratibu wa Elimu kuongoza. Viongozi wote wamekosa uwajibikaji na wanatumia mamlaka waliyopewa vibaya.

Mkuu wa Wilaya ni fisadi, mbinafsi na mtu mwenye tamaa. Anajali maslahi yake binafsi na ya familia yake. Anapokea hongo kutoka kwa wafanyibiashara na kuwalazimisha kumpatia zawadi wakati wa sikukuu za Pasaka, Mtakatifu Antoni na Mtakatifu Basili. Anapora pesa zilizotolewa kujenga kanisa la hospitali. Aidha hafanyi lolote kuhakikishia raia usalama wao. Anatumia polisi kuwakandamiza wanyonge. Wafanyibiashara wakikataa kumpa zawadi wanachapwa, kuvutwa ndevu, kutusiwa au kulishwa kauzu za chumvi na polisi. Aidha, mke wa Sajeni anachapwa na polisi kwa tuhuma za kupigana hadharani sokoni. Ameshindwa kabisa kuwa kielelezo bora kwa viongozi wengine wanaofanya kazi chini yake.

Viongozi wanaosimamia idara mbalimbali wameiga tabia na mwenendo wa kiongozi wao. Hakuna hata mmoja anayetekeleza wajibu wake inavyopasa. Bw. Huruma, kiongozi anayesimamia hospitali hashughulikii maslahi ya wagonjwa wanaolazwa hospitalini. Amemwajiri Heibna kuwatibu wagonjwa. Daktari huyu hawezi kusema hata neno moja la Kirusi. Hakuna mawasiliano yoyote yanayoendelezwa baina ya daktari na wagonjwa. Wagonjwa waliolazwa ni wengi mno aidha hawapati matibabu yoyote kwa kuwa wao ni wa tabaka la chini. Vifo vya wagonjwa havimpatii wasiwasi. Habari za kufika kwa

Mkaguzi Mkuu zinapowafikia, wagonjwa wanafukuzwa kutoka hospitalini. Wamebaki kumi tu. Bw. Huruma hataki kupata sifa mbaya. Anataka kuonekana kuwa anafanya kazi yake vyema. Wagonjwa wanaougua maradhi mbalimbali wanarundikwa pamoja katika wadi moja. Isitoshe, malazi na mavazi ya wagonjwa hayasafishwi, ni machafu kwelikweli.

Mahakama imejaa uozo. Bw. Hakimu ni mfisadi. Anachukua hongo kutoka kwa watuhumiwa. Aidha amepanga kujinufaisha kutokana na kesi inayowakabili Cheptovichi na Valinski. Amepanga kulipeleka jibwa lake kuwinda katika bustani ya Valinski siku moja na ya Cheptovichi siku inayofuata. Ofisi za mahakama ni chafu mno, zimejaa ngozi zilizotundikwa ili zikauke. Mijeredi na vifaa vingine vya kuwindia vimerundikana ovyo. Rekodi za Mahakama hazihifadhiwi vizuri. Wafungwa hawalishwi. Tunaelezwa kuwa hawajala kwa muda wa majuma mawili. Karani wa mahakama ni mlevi kupindukia. Anaendesha kesi mahakamani akiwa mlevi. Aidha amegeuza ofisi za mahakama na kuzifanya kuwa vibanda vya kufugia kuku, bata na ndege.

Mkuu wa idara ya posta anatumia mamlaka yake vibaya. Hana maadili anaposhughulikia barua za wateja wake. Yeye huzifungua na kuzisoma na anapopata barua ambazo zina malalamiko dhidi yao, anazihifadhi na kukosa kuzituma kabisa.

Mratibu wa elimu amepewa wajibu wa kuwasimamia walimu. Gogol anatueleza kuwa walimu wake wamehitimu lakini wana tabia ya ajabu. Wanakunja nyuso zao wanapofundisha na kuharibu mali ya shule. Mkuu wa Wilaya anamtaka awashauri walimu wake ili warekebishe mienendo yao mibaya. Anasema:

> **MKUU WA WILAYA:** Ndiyo, ndiyo. Na sasa mchukue mwalimu wa historia. Ni mtu mwenye uwezo mkubwa sana anayejua somo lake barabara, lakini anafundisha kwa mori kiasi cha kuwa huwezi kumwelewa. Nilipata kumsikiliza kwa mara moja, alipokuwa akizungumza juu ya Waasiria na Wababelonia alikuwa sawa, lakini alipofika Alekzanda Mkuu hungeweza kuamini kabisa. Nilidhani kuwa mahali panaungua moto. Aliruka kutoka mezani mwake, akatwaa kiti na kukibamiza chini, halafu akakiinua juu na kukizungusha juu ya kichwa chake! Nadhani alikuwa anaelezea juu ya vita. Ni kweli kuwa Alekzanda alikuwa Jenerali Mkuu na mengine mengi lakini kwa nini avunje vitu, mali ya serikali? (Uk.5)

Mkuu wa Polisi naye hana uthibiti wowote kwa polisi anaowasimamia. Askari hawa

wanafika kazini wakiwa walevi na wanakimbiakimbia ovyo mjini wakiwa nusu uchi. Askari wengine hawafiki kazini kabisa kwa sababu ya ulevi.

Mkuu wa Wilaya, Bw. Hakimu, Bw. Huruma na Mratibu wa Elimu wana kila sababu ya kushtuka wanapopata fununu kuwa Mkaguzi Mkuu kutoka Pitasbag anakuja kisirisiri bila kujitambulisha kuukagua mkoa. Wanafahamu kuwa hawatekelezi wajibu wao vyema. Mji ni mchafu na vitengo wanavyosimamia vimejaa uozo. Hofu yao ni kubwa mno mpaka inawafanya wamkosee kijana aliyevalia kisasa na mwenye maringo kuwa ndiye Mkaguzi Mkuu. Ghlestakovu ni kijana wa umri wa miaka ishirini na mitatu. Yeye ni karani mdogo kutoka Pitasbag. Yumo safarini kwenda kumwona babake huko shamba katika mkoa wa Saratovu. Ghlestakovu amepoteza fedha zake zote kwa mchezo wa kamari na anaishi maisha duni katika hoteli moja mjini.

Mkuu wa Wilaya akihofu kuwa Mkaguzi Mkuu amefika, anawaita maofisa wa idara mbalimbali katika mkutano wa dharura ili kujadili athari za habari hizi. Mambo wanayojadiliana katika mkutano huo yanadhihirisha ukosefu wa uwajibikaji, matumizi mabaya ya mamlaka na ufisadi unaoendelezwa na maofisa hawa wa ngazi mbalimbali ambao wana kila sababu ya kushtuka wanapotajiwa kuwa Mkaguzi Mkuu amefika. Wakiwa wanaendelea na mazungumzo kuhusu mikakati ambayo wanaweza kutumia kuficha uozo katika idara wanazosimamia, Bw. Posta anaingia. Mkuu wa Wilaya anamshauri kuzifungua barua zote zinazopitia mikononi mwake na kuzisoma. Anaagizwa kuzitupa zile zilizo na malalamiko dhidi yao na kuzituma zisizokuwa na husuda yoyote kuwahusu. Kabla ya kumalizika kwa mkutano, Bobchinski na Dobchinski wanaingia kwa kishindo. Wanaleta habari za kuwatia kiwewe zaidi. Wamemwona kijana katika hoteli moja mjini aliye na tabia ya ajabu kabisa. Amekuwa hapo kwa muda wa majuma mawili, haonyeshi dalili za kuondoka na anachukua kila kitu kwa mkopo na halipi hata senti moja. Mkuu wa Wilaya na maofisa wenzake wanakubaliana kuwa aliyeonekana ndiye Mkaguzi Mkuu.

Mkuu wa Wilaya anamaliza mkutano upesi na anaondoka kwenda hotelini kukutana na "Mkaguzi Mkuu" akiwa na nia ya kumhonga ili apatane naye. Afikapo hotelini, anaanza kufanya upelelezi kuhusu kijana aliyeonekana huko. Ghlestakovu anapopata habari za upelelezi huo kupitia mtumishi wake Yosif, anashtuka na kuwaza kuwa mwenye hoteli tayari amemshtaki kwa kutomlipa deni lake la malazi na maakuli. Mkuu wa Wilaya anafanikiwa kumhonga shilingi mia nne na kumpa mwaliko wa kutembelea mashirika

mbalimbali hapo mjini. Aidha anamkaribisha kwake ambapo anampa chakula na malazi.

Ghlestakovu na Mkuu wa Wilaya wanarudi nyumbani baada ya kuzuru shirika la afya na baada ya kupata chakula cha mchana katika hospitali. Mkewe Mkuu wa Wilaya na bintiye wanafurahi kumkaribisha mgeni wao maarufu. Mkuu wa Wilaya na Bw. Huruma wanajisifu mbele ya mgeni kuhusu mafanikio yao na uwajibikaji wao kazini. Wenyeji wanampa mgeni wao pombe mpaka anaanza kuporokwa ovyo. Mgeni anawadanganya wenyeji wake kuwa yeye ni mwandishi na mtu maarufu sana aliye na uwezo wa kutangamana na maofisa wa ngazi za juu zaidi kama mabalozi na mawaziri mjini Pitasbag. Wasikilizaji wake ni wepesi wa kudanganyika na wanaamini kila wanaloambiwa.

Siku inayofuata, maofisa wengi wanafika nyumbani kwa Mkuu wa Wilaya. Wana hamu kubwa ya kutaka kuzungumza na “Mkaguzi Mkuu”. Wanapanga foleni nje ya chumba chake na kuingia mmoja mmoja kuzungumza naye kisha kuondoka baada ya kumpatia hongo. Ghlestakovu sasa amegundua kuwa maofisa hawa wamekosea kwa kumchukulia kuwa mtu maarufu. Anatia makali mchezo wake na kujinufaisha zaidi kutokana na hali hii. Anaomba mikopo kutoka kwa Mratibu wa Elimu, Bw. Hakimu na Bw. Huruma. Anawasikiliza kwa mshangao jinsi maofisa hawa wanavyolaumiana mbele yake. Baada ya kuhisi kufanikiwa anaamua kumwandikia rafikiye Ryapitikini barua kumweleza kuhusu vituko alivyoshuhudia akiwa safarini. Anamwelezea namna alivyokutana na maofisa wapumbavu na jinsi alivyojinufaisha kutokana na ushenzi wao. Yosif anamtaka waondoke pale mjini lakini kabla ya kuondoka, anawakaribisha wafanyibiashara. Anasikiliza manung’uniko yao dhidi ya Mkuu wa Wilaya na kujipatia zawadi zaidi.

Ghlestakovu anaamua kuondoka kwa siku chache baada ya kumposa bintiye Mkuu wa Wilaya. Kichwa chake kikiwa kimejaa pombe na kumbukumbu za starehe, anamdanganya Mkuu wa Wilaya kuwa anataka kwenda kumwona mjomba wake ile ampe baraka zake katika ndoa anayopanga. Akijisikia kufanikiwa, Mkuu wa Wilaya anageuka kuwa mkaidi zaidi, mwonevu zaidi na mnyang’anyi zaidi kuliko awali. Anaona fahari kubwa mno kuwa na mkwe mashuhuri. Anaanza kuota kuwa atakuwa mtu maarufu sana. Wageni wengi wanafika nyumbani kwa Mkuu wa Wilaya kuleta pongezi zao baada ya kupata habari kuwa bintiye kaposwa na “Mkaguzi Mkuu”. Wakati ambapo wageni wanaendelea na shamrashamra hizi, Bw. Posta anawasili akiwa ameinua barua juu. Anaisoma kwa sauti wote wakiwa wanamsikiliza kwa makini. Wanapigwa na butwaa

wanapotambua kuwa wamedanganywa na wangali wanazungumza kwa chuki kumkemea na kumlaani Ghlestakovu, anapoingia askari na tangazo kuwa Mkaguzi Mkuu amewasili na anataka kumwona Mkuu wa Wilaya mara moja.

### 3.3 Msuko katika *Mstahiki Meya.*

Tamthilia ya Mstahiki Meya inahusu utawala wa Mstahiki Meya ambaye ni kiongozi anayesimamia Baraza la mji wa Cheneo. Umma unawateua viongozi wao ukiwa na matumaini kuwa wataboresha maisha yao na kusaidia kufikia viwango vya juu vya maendeleo. Mstahiki Meya anasahau wajibu aliotwika na umma. Anaungana na Diwani I, Diwani II na Bili kupora mali ya umma.

Mstahiki Meya hajali maslahi ya wanyonge. Baada ya kushika usukani anaanza kutafuta mianya ya kujilimbikizia mali. Ananyakua vipande vinane vya ardhi vingine anamgawia rafikiye Bili. Meya ana mpango wa kumtimua mwanakandarasi aliyekuwa amepatiwa kandarasi na Meya aliyemtangulia. Anamshauri kulishtaki Baraza ili alipwe fidia kisha amgawie kiasi fulani cha fidia hiyo. Aidha anaunga mkono pendekezo la Bili la kuuza fimbo ya Meya. Yeye hapingi lolote analoshauriwa na Bili na hawezi kufanya maamuzi yoyote ya busara bila kutafuta ushauri kwake.

Madiwani wa Baraza la mji wa Cheneo wanaunda sheria zinazowanufaisha viongozi na kuwakandamiza raia. Meya, Diwani I na Diwani II wanapitisha sheria ya kutotozwa kodi kwa mishahara yao ilhali tunaona kuwa wafanyikazi wanaolipwa mishahara duni wanatozwa kodi. Aidha wanakubaliana kujipatia nyongeza ya mishahara hata kama uchumi wa Baraza haumudu kugharamia mishahara hiyo. Zaidi ya hayo, wanaunga mkono pendekezo la kuundwa kwa kamati za madiwani ambazo hazina manufaa yoyote kwa Baraza.

Viongozi wanafuja pesa za umma bila kujali. Mstahiki Meya anatumia *entertainment vote* kujistaheresha na kuwastaheresha marafiki. Anampeleka Bili na familia yake kula na kunywa katika hoteli ya Kajifahari. Amepanga kuwapa mameya ambao wanakuja kuzuru mji wa Cheneo makaribisho ya kupigiwa mfano: hoteli za kifahari, vyakula kutoka tamaduni zote aidha amepanga kuagiza mvinyo na divai kutoka ng’ambo. Anamlipa Mhubiri shilingi laki moja kila mwezi na kugharamia petroli ya kumleta barazani na kumrudisha nyumbani. Anawalipa madiwani I na II ovataimu na marupurupu baada ya kuketi katika mkutano na kupanga namna ya kuuza fimbo ya Meya. Isitoshe, Meya

anamlipa Bili kwa huduma ambazo hajatoa. Yeye si mfanyikazi wa Baraza. Mstahiki Meya anafanya haya yote wakati ambapo wafanyikazi maskini wa Baraza wanakufa kwa kula mizizi na matunda ya mwitu.

Kwa sababu ya matumizi mabaya ya fedha, Baraza halina pesa. Lina nakisi ya shilingi milioni mia moja na ishirini. Baraza limeshindwa kulipa mishahara ya wafanyikazi. Linategemea mikopo kutoka nchi za Ulaya. Mikopo hii inapopatikana, inatumika kiholela kulipa mishahara ya madiwani. Meya hajali kuachia vizazi vijavyo mzigo mkubwa wa kuilipia kwa riba.

Sekta ya elimu nayo imeathiriwa vibaya. Elimu wanayopata watoto wa maskini ni duni mno. Ni ya kukariri mawazo. Madaktari hata baada ya kuhitimu hawawezi kutekeleza kazi yao vyema. Viongozi wa Cheneo hawana mipango yoyote ya kutaka kuimarisha viwango vya elimu. Wao huwapeleka watoto wao kusoma ng’ambo hata matibabu wanakwenda kuyatafuta huko. Tunaelezwa kuwa Mstahiki Meya amewapeleka watoto wake kusomea ng’ambo hata mke wake anaenda hospitali za ng’ambo kujifungulia huko. Hataki kubahatisha kwani madaktari wa Cheneo ni wa kubabaisha tu kama anavyodai. Aidha tunaelezwa kuwa kuna vijana wengi ambao wamehitimu kutoka vyuo vikuu lakini hawana ajira. Viongozi wa Cheneo hawana mikakati yoyote ya kubuni nafasi za ajira kwa vijana waliohitimu.

Arege anatueleza mbinu zinazotumika na viongozi kujidumisha mamlakani. Mstahiki Meya anatumia vitisho, polisi, ubaguzi, hongo, vishawishi na propaganda. Meya anambagua Diwani III kwa kuwa ni mwadilifu na anatetea maslahi ya wafanyikazi. Anakerwa mno anapoona wananchi wakidhalilishwa na viongozi. Mikutano mingine inafanywa bila ya yeye kupata mwaliko. Meya anawadanganya Waridi na Siki kuwa shehena ya dawa iko njiani. Anawahonga askari kwa kuwapatia asilimia ishirini ya nyongeza ya mishahara. Wafanyikazi wa Baraza wanapogoma kudai nyongeza ya mishahara, anawatisha kuwa atawafuta kazi na kuwaajiri vijana waliohitimu hivi karibuni kutoka vyuo vikuu. Aidha anatuma askari kuwafurusha kwa kuwapiga, kuwafyatulia risasi na kuwatupia vitoa machozi. Isitoshe, Meya anaamrisha idhaa ya Baraza kucheza nyimbo za uzalendo kabla na baada ya vipindi maarufu. Hii ni njia ya kuwapumbaza wananchi na kuwafanya kufikiria kuwa kila kitu kilikuwa sawa.

Uongozi wa Mstahiki Meya umewatelekeza wanyonge katika njaa na umaskini mkubwa. Wafanyikazi wanaolitumikia Baraza wanapitia matatizo chungu mzima: Wanalipwa

mishahara duni, mishahara yao inacheleweshwa na wakati mwingine wanalipwa mishahara nusu. Kwa sababu ya malipo duni, hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi, elimu na matibabu. Tunaelezwa kuwa mamake Dadavuo Kaole anampa mtoto mabaki ya chakula anayobeba kutoka kwa mwajiri wake pia wanakula chakula cha mbwa. Watoto wa maskini wanatembea kwa miguu kwenda shuleni. Wafikapo shuleni wanafukuzwa kwa kukosa kulipa karo. Watoto wa madiwani wanapelekwa shuleni kwa magari makubwa makubwa ya serikali yaliyo na *air conditioner*. Wafanyikazi wanaishi katika mabanda. Madiwani wanaishi katika makasri ambayo yamesheheni kila aina ya mapambo. Wafanyikazi hawawezi kumudu gharama ya matibabu. Wao pamoja na watoto wao wanakufa kwa kukosa matibabu. Tunaelezwa kuwa Dadavuo Kaole anaaga dunia. Meya anapoelezwa kuhusu kifo cha mtoto, anasema kuwa huyo ni mmoja tu na kwamba Cheneo ina watu wengi. Isitoshe, wafanyikazi wanafanya kazi katika mazingira duni. Hawana vifaa muhimu vya kufanyia kazi.

Maisha ya wafanyikazi yanaendelea kuwa mabaya zaidi. Mstahiki Meya hataki kuwapatia nyongeza ya mishahara. Baraza lina pesa za kuwapa madiwani lakini halina pesa za kuwapatia wanyonge. Ukatili ulioje! Daktari Siki na Diwani III wanajaribu kumkumbusha Meya kuhusu wajibu wake wa kuyaboresha maisha ya watu waliomchagua. Hataki kuwasikiliza. Anawasikiliza sana Bili, Diwani I na Diwani II ambao wanamdanganya. Wafanyikazi wamechoka kudhulumiwa. Wamekata shauri kutorudi kazini bila nyongeza ya mshahara. Meya amekuwa akipuuza nguvu za wanyonge ambao wameamua kutouza huduma yao kwa Baraza kwa bei ya chini. Wafanyikazi wa bohari la mafuta na wale wanaofanya kazi katika uwanja wa ndege nao wanagoma ili kuwaunga mkono wenzao wanaogoma. Mji ni mchafu. Mahoteli hayana maji safi yanayoweza kufikia viwango vya kimataifa. Hali ya uchafu Cheneo imesababisha safari ya wageni kuahirishwa kwa kuhofia kuzuka kwa maradhi ya kipindupindu. Mstahiki Meya na Diwani II wanahisi kuwa pana haja ya kutumia nguvu kuwashurutisha wafanyikazi kurudi kazini. Meya anaapa kutumia nguvu kurejesha hali ya kawaida.

Hali hii ya taharuki ikiendelea, askari wawili wanaingia katika ofisi ya Meya wakiwa wamebeba bunduki. Meya anapowaona anafurahia sana na kuwashukuru kwa kufika kila anapowahitaji. Hata hivyo, wanamwarifu kuwa wageni waliowatarajia kwa hamu na ghamu wameahirisha safari yao. Madiwani wanafurahia ripoti hiyo. Lakini askari wanatoa taarifa nyingine kuwa walikuwa wametumwa na makao makuu kuja

kuwakamata. Walitakiwa kwenda kueleza sababu za hali ya mambo kuwa vile yalivyokuwa. Mstahiki Meya ambaye amezoea kutowajibikia makosa yake anakana ukweli wa mambo haya na kudai kuwa yametiwa chumvi na vyombo vya habari. Uzito wa jambo hili unamfanya Meya kuzirai na kuanguka kutoka kitini. Askari wanawakamata Diwani I na Diwani II na kuwatia pingu. Lililo na mwanzo halikosi kuwa na mwisho. Uongozi dhalimu wa Mstahiki Meya unafika tamati.

### 3.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumefafanua kipengele cha msuko katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* na kudhihirisha kuwa tamthilia zote mbili zinasemezana kwa mujibu wa Mikhael Bahktin. Misuko yote ni sahili. Matukio yanafuatana moja kwa moja kuanzia kitendo cha kwanza, cha pili, cha tatu hadi cha mwisho. Aidha misuko yote inahusu uongozi dhalimu na matumizi mabaya ya mamlaka ya viongozi Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya. Waandishi Timothy Arege na Nikolai Gogol wanadhihirisha wazi kuwa uongozi unaowakandamiza raia haudumu. Isitoshe, msuko katika *Mstahiki Meya* una sifa ya kuwa na visababishi na ule wa *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* una sifa ya kitashtiti.

# SURA YA NNE

# MWINGILIANOMATINI KATIKA UHUSIKA NA MANDHARI

## 4.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumetathmini na kuhakiki vipengele viwili vya kimwingilianomatini. Vipengele hivi ni wahusika na mandhari. Wahusika wanaopatikana katika kazi za kifasihi aghalabu huingiliana. Waandishi tofautitofauti huweza kuwasawiri wahusika wao kwa njia zinazoshabihiana kwa njia moja au nyingine. Aidha wahusika wanaweza kuingiliana kisifa, kimtazamo na hali kadhalika kimwono-ulimwengu. Wahusika huingiliana katika harakati za kuyatekeleza majukumu fulani wanayopatiwa na msanii.

Katika kazi za kifasihi, wasanii hutuchorea wahusika wa aina nyingi (Kimani na Chimerah (1999) Wameainisha wahusika wakizingatia kigezo cha sifa kama ifuatavyo: wahusika wa miraba minne na wahusika wa mraba mmoja. Wahusika wa miraba minne wana sifa nyingi. Nyingine zikiwa nzuri na nyingine zikiwa mbaya. Maisha ya wahusika wa aina hii ni mapana katika tajriba na matukio. Wahusika wa mraba mmoja ni wale ambao huwa na sifa moja tu na hawabadiliki. Naye wamitila (2002) akimnukuu Forster (1927) alisema kuwa, Forster aligawa wahusika wa fasihi kwa kutumia ‘sitiari’ mbili maarufu; ubapa na uduara. Wahusika wanaweza kuwa duara au bapa. Walio bapa huwa hawabadiliki tangu mwanzo hadi mwisho. Ikiwa mhusika ni mbaya anabakia na sifa zizo hizo hadi mwisho wa hadithi. Kwa upande mwingine, ikiwa mhusika ni mzuri basi anadumisha sifa hizo katika hadithi nzima. Wahusika duara nao ni wale ambao kwa kiasi kikubwa wanakaribiana na binadamu wa kawaida. Forster alisema kuwa msingi mkuu wa kuwabaini wahusika hawa ni uwezo wao wa kuweza kutushtukiza au kutushangaza. Uduara wao umo kwenye mabadiliko yanayowajia. Mabadiliko haya yanaweza kuwa ya kitabia, kimawazo kijamii kiukuaji na kadhalika. Matendo na maisha yao yanaongozwa na hali halisi. Wanajibainisha kwa mapana na marefu yao kihisia na kimatendo. Hawa ndio wahusika wanaovutia zaidi kwa sababu wanaisukuma riwaya au tamthilia mbele.

Katika uhakiki wetu, tumejikita kudhihirisha jinsi wahusika wa tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu* na *Mstahiki Meya* wanavyoingiliana kwa mujibu wa sifa ambazo tumetangulia kuzitaja. Aidha tumedhihirisha jinsi tamthilia hizi zinavyoingiliana kwa mujibu wa mandhari.

### 4.2 Mwingilianomatini katika uhusika

Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* zinaingiliana kiwahusika. Katika sura hii, tumeonyesha jinsi wahusika mbalimbali wanavyoingiliana na kuchangizana.

#### 4.2.1 Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya

Nikolai Gogol na Timothy Arege wametusawiria wahusika hawa wawili kwa njia zinazolandana. Wote wawili ni viongozi. Mkuu wa Wilaya ni kiongozi wa polisi na usalama naye Mstahiki Meya ni mkuu wa Baraza la mji wa Cheneo. Wote wawili wana familia. Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya wanalandana kihulka. Wote wawili ni wafisadi. Mstahiki Meya amenyakua viwanja vinane vya ardhi na vingine vinne amemgawia Bili. Meya anasema:

> **Meya**: Nisipokuwa nazo, nani atakuwa nazo? Mimi nimeuza vipande vyangu vitatu vya ardhi kupata pesa kwa ajili hii. Nimebakiza vitano *incase*. Wewe nilikugawia vinne unaweza kuuza kimoja au viwili kwa ajili hiyo, vingine viweke kwa ajili ya hao watoto unaowahangaikia, hasa ile *prime plot.* (Uk. 27)

Mstahiki Meya amepanga njama nyingi za kujipatia fedha. Anakubali kushtakiwa kwa Baraza na mwanakandarasi ili afaidike kwa fungu atakalopewa na mwanakandarasi. Bili anapopendekeza wauze fimbo ya Meya ambayo ni dhahabu tupu, anakubali upesi kwa masharti kuwa hiyo itakuwa siri yao hadi kifo. Aidha, Meya anampigania mhazili wake mpaka anapata kazi ambayo hakustahili. Anaunda mabaraza ya kuhudumu ambayo anataka kuyatumia kama mwanya wa kulifisidi Baraza. Zaidi ya hayo, Diwani III anatueleza kuwa umeya hauna pato kubwa ila ofisi ndiyo iliyo na mianya mingi ya kujipatia utajiri.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya amepanga kuwahonga askari ili wakubali kuonyesha kuridhika kwao mbele ya Mkaguzi Mkuu. Vilevile, anawalazimisha wafanyibiashara kumpatia kilo hamsini za nta na zawadi wakati wa sikukuu ya Pasaka, sikukuu ya Mtakatifu Antonio na Basili. Malalamiko ya wafanyibiashara yanadhihirisha hili:

**ABDULINI**: Na Mkuu wa Wilaya. Hajatokea Mkuu wa Wilaya kama yeye, anatunyanyasa kwa kututumia askari wenye rungu. Sasa hakuna kilichotubakia ila kamba shingoni mwetu (*akiigiza kujinyonga*) na kufa. Tabia yake imekosa busara kabisa. "Nyie makapi!" Mungu shahidi yangu! Kama tungekuwa tumemwudhi kwa lolote, lakini daima tumefanya kinachotegemewa. Nguo kwa mkewe na bintiye, zawadi wakati wa pasaka, hivyo vyote hatujali! Lakini hata hivyo haridhiki.

**M/BIASHARA 3**: … Mtakatifu Antoni ni siku ya jina lake, na halafu tunampelekea kila aina ya vitu. Lakini hilo halitoshi. Anasema Mtakatifu Basili pia ni siku ya jina lake na tunapaswa kumpa zawadi siku hiyo pia. (uk. 54-55)

Isitoshe, Mkuu wa Wilaya amepora pesa zilizotolewa na serikali kuu miaka mitano iliyopita kujenga kanisa la hospitali. Anamtaka Mkuu wa Polisi amweleze Mkaguzi Mkuu kuwa kanisa lilianzishwa lakini kwa bahati mbaya likachomeka. Aidha tunapata habari kuwa mwana wa fundi wa cherahani na wa mshona urembo ni vijana ambao hawajaoa na kulingana na sheria za nchi ya Urusi, makapera walipaswa kusajiliwa kujiunga na kikosi cha wanajeshi ili waende kupigana vitani. Kwa kuwa wazazi wao walihofia maisha ya watoto wao kwenda kupigana vitani, wanamhonga Mkuu wa Wilaya ambaye anasitisha mpango huu wa kuwasajili na kumshurutisha Mhunzi ambaye ameoa kujiunga na kikosi kinyume na sheria. Hali kadhalika, anakiri mbele ya Ghlestakovu kuwa yeye huchukua hongo kwa sababu mshahara anaopokea ni mdogo zaidi. Aidha, anamhonga Ghlestakovu kwa kumpa shilingi mia nne.

Mstahiki Meya na Mkuu wa Wilaya ni wadanganyifu. Mstahiki Meya anawadanganya wafanyikazi wa Baraza kuwa ameagiza dawa. Isitoshe, anapanga kuiba fimbo ya Meya na kuiuza ng'ambo. Baada ya kutekeleza hili, anapanga kuwaeleza wafanyikazi kuwa fimbo ilipotea wakati wa vurugu kutokea barazani.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya anamtaka Mkuu wa Polisi kusema uongo kuhusu pesa zililotolewa miaka mitano iliyopita kujenga kanisa la hospitali. Zaidi ya hayo, anapogundua kuwa amedanganywa na Ghlestakovu anatueleza kuwa hajawahi kudanganywa maishani ingawa amewahi kuwalaghai watu wengi wakiwemo majangili na majambazi ambao wangeweza kuiba dunia nzima.

Viongozi wote wawili wana tamaa na ubinafsi mkubwa. Mstahiki Meya amejilimbikiza mali nyingi wakati ambapo wananchi wanateseka. Chakula chake na mapambo ya

nyumba yake ni ishara tosha ya maisha ya kifahari aliyokuwa akiishi. Kwingineko tunaelezwa kuwa watoto wake wanasomea ng'ambo huku mkewe akitafuta matibabu huko. Meya anaidhinisha nyongeza ya mishahara ya madiwani kwa kuwa anataka kunufaika. Anakubali kuuza fimbo ya Meya kwa tamaa ya pesa. Anaunda kamati za madiwani kwa tamaa ya uongozi. Anataka kuungwa mkono na viongozi wa kamati hizi. Hali kadhalika, anakubaliana na mpango wa Bili wa kujipatia pesa kutokana na mwanakandarasi.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya anashiriki ufisadi ili kujipatia fedha na mali. Anawashurutisha wafanyibiashara kumpa mavazi ya mkewe na bintiye. Aidha, anatoa zabuni kwa wafanyibiashara ambao wanampatia milungura.

Viongozi wote wawili hawajali maslahi ya raia. Wanacheneo wanakufa kwa kula matunda na mizizi ya mwitu. Daktari Siki anapomweleza Mstahiki Meya kuhusu kifo cha mtoto Dadavuo Kaole, anasema kuwa huyo ni mmoja tu eti Cheneo ina watu wengi. Aidha anafurahia kutawanywa kwa wafanyikazi na polisi. Anacheka na kusema kuwa huo ni msiba wa kujitakia ambao hauna kilio. Mkuu wa Wilaya naye anatoa amri ya kudhulumiwa kwa wafanyibiashara wowote ambao wanatoa manung'uniko dhidi yake. Aidha, anatisha kufunga maduka ya wale ambao wanakataa kumhonga.

Mstahiki Meya na Mkuu wa Wilaya ni wanafiki. Wanajifanya wameokoka lakini matendo yao ni mabaya. Ni fisadi, na wamejawa na tamaa. Mstahiki Meya anamwambia Mhubiri kuwa kila wakikutana kitu humsukuma kutaka kumfuata. Hata mara mbili karibu aache kazi yake ya umeya aungane naye kueneza injili. Aidha, anatoa amri kwa kinara wa uhusiano mwema kuwachezea watu nyimbo za kizalendo kabla na baada ya vipindi maarufu vya redio. Anatumia nyimbo hizi kama ujanja wa kuridhisha roho za raia na kuwasahaulisha dhuluma anazowafanyia. Anataka kuwapumbaza wanacheneo. Anaunda kamati za kuhudumu akiwa na nia ya kuwateka akili madiwani wengi kumuunga mkono na anahakikisha kuwa madiwani wenye ushawishi mkubwa wameteuliwa ili kuongoza kamati hizi. Anataka zidhibitiwe kulingana na maslahi yake. Hali kadhalika, Meya anamsifu Bili kwa pendekezo lake la kumtaka kushirikiana na mwanakandarasi kuliibia Baraza. Anamwambia kuwa haishi kumshangaza kwa namna akili yake inavyofanya kazi. Huu ni unafiki tu wa kumvuta Bili kwake.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya anajipiga kifua mbele ya Ghlestakovu akieleza namna alivyothibiti uongozi ilhali tunafahamu kuwa hajawajibika. Kadhalika,

anamweleza kuwa ametembea hotelini kwa sababu ya upendo wa Yesu alio nao kwa wasafiri kuhakikisha kuwa wamepokelewa vyema. Ukweli ni kwamba amefika pale hoteni kutafuta njia ya kumhonga. Isitoshe, anamweleza kuwa yeye si kama wakuu wa wilaya na viongozi wengine ambao wanajali zaidi shughuli zao za kibinafsi. Yeye hataki sifa mradi tu mji unatunzwa vyema, mitaa inakuwa safi, wafungwa wanatunzwa vyema na ulevi umepunguzwa. Hiki ni kinaya kwa kuwa tunafahamu kuwa mji ni mchafu, wafungwa hawatunzwi na wafanyikazi wake ni walevi.

Viongozi wote wawili ni dhalimu. Mstahiki Meya anawalipa wafanyikazi mishahara duni. Wafanyikazi hawa wanapogoma kudai nyongeza ya mishahara, anawatuma polisi kuwapiga na kuwatupia vitoa machozi. Aidha, tunaelezwa kuwa hakuna dawa katika zahanati na wagonjwa wanakufa kwa kukosa matibabu. Wanyonge wanaolazwa kwenye zahanati wanatarajiwa kulipa licha ya kuwa hakuna dawa. Mbali na hayo, anafuja hazina ya Baraza kwa kuidhinisha malipo yasiyofaa kama vile: nyongeza ya mishahara na marupurupu kwa walinda usalama na madiwani, kutoa sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi kwa Mhubiri, kulipwa ovataimu kwa Diwani I na Diwani II na kumlipa Bili kwa huduma asiyotoa.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya anawashurutisha wafanyibiashara kumpa zawadi. Vilevile, anawatuma polisi kuwachapa wale wanaotoa malalamiko dhidi yake. Isitoshe, anafunga maduka yao bila sababu maalum. Hali kadhalika, anawashurutisha wanyonge kujiunga na kikosi cha wanajeshi.

Aidha, viongozi wote wanatumia mbinu zinazofanana katika uongozi wao. Wanatumia propaganda, vitisho na polisi. Mstahiki Meya anatumia propaganda kuwashawishi raia kumuunga mkono. Anamweleza Daktari Siki kuwa hata akitaka kuchaguliwa mara ya nne, tano na sita watu watamchagua kwani ana akili. Anawadanganya Daktari Siki na Waridi kuwa tatizo la dawa linashughulikiwa ili aonekane kuwa amewajibika. Anawapa wawakilishi wa wafanyikazi nafasi ya kukutana naye kama mbinu ya kuwafanya wahisi wanathaminiwa. Baada ya mkutano, anawaahidi kwamba atawaeleza madiwani kuhusu manung'uniko yao. Huu ni uongo tu wa kuwatuliza. Hali kadhalika, anaidhinisha kuandaliwa kwa tamasha za vijana kushindania zawadi kwa kubuni na kucheza nyimbo. Hii ni hila inayonuia kuwafanya vijana kuhisi kuwa wanathaminiwa kwa kutunukiwa zawadi na kuonyeshwa kwenye vyombo vya habari pia anatumia vitisho kuwashinikiza raia kumuunga mkono. Anamtisha Siki na kumfurusha kutoka nyumbani kwake.

Anamweleza kuwa anatia kidole chake katika mzinga wa nyuki kwa kujaribu kumweleza kuwa ni vyema kusikiliza malalamiko ya wafanyikazi. Anawatisha Beka, Tatu na Medi kwamba hatakubali matamshi yao ya kuliumbua Baraza. Isitoshe, wafanyikazi wanapogoma, polisi wanaamrishwa kuwafurusha kwa kuwapiga kwa marungu na kuwatupia vitoa machozi.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya naye anatumia mbinu zizo hizo kuongoza. Anawatisha wafanyibiashara kuwa atafunga maduka yao iwapo watakataa kutekeleza matakwa yake ya kumhonga. Aidha anawaamrisha askari kuwadhulumu raia wasiokuwa na hatia.

Mbali na hayo, Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya ni viongozi wanaopenda kulinganisha uongozi wao na wa viongozi wengine. Daktari Siki anapomtembelea Mstahiki Meya na kumweleza masaibu yote yanayowakumba wafanyikazi, Meya anamweleza kuwa hakuna baraza lingine lenye uthabiti na maendeleo kama lile analoongoza. Naye Mkuu wa Wilaya anamwambia Ghlestakovu kuwa yeye ni kiongozi aliyewajibika. Anajisifu na kujigamba kuwa yeye si kama wakuu wa wilaya wengine ambao wanatanguliza maslahi yao mbele.

Mstahiki Meya na Mkaguzi Mkuu ni viongozi waoga. Daktari Siki anakwenda kwa Meya kumweleza matatizo yanayowakabili wafanyikazi. Punde tu anapotoka nyumbani, Meya anaandaa mkutano wa dharura na madiwani kwani anayoelezwa na Daktari Siki yamemtisha. Aidha, anatishika sana wakati ambapo wawakilishi wa wafanyikazi wanapokuwa na msimamo thabiti kuhusu swala la kuendelea na mgomo wao. Anafahamu kuwa wanaweza kuwa tishio kubwa kwa safari ya mameya wanaotarajiwa. Hali kadhalika, Mstahiki Meya na Mhubiri wanapoendeleza maombi yao kwa sauti ya juu, askari wanafikiria kwamba Meya anashambuliwa na wafanyikazi wanaogoma. Wanaingia ofisini na kuamrisha kila mtu kulala chini. Meya analala chini na kuinua mikono juu. Tendo hili la maafisa wa usalama linaibua ucheshi ambao hasa unadhamiria kuwasuta Meya na Mhubiri kwa kutumia ofisi za umma kwa maslahi yao ya kibinafsi. Isitoshe, anaogopa hadi anaanguka chini na kuzirai askari wanapokuja ofisini mwake na kumweleza kuwa wametumwa kuja kumkamata.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya anadhihirisha sifa iyo hiyo. Anaogopa anapopata habari kutoka kwa rafikiye Atemi Chimihovu kuwa Mkaguzi Mkuu kutoka Pitasbag anakuja kisirisiri bila kujitambulisha kuja kuukagua mkoa. Anaandaa mkutano

wa dharura na Bw. Hakimu, Bw. Huruma na Mratibu wa Elimu kwani habari hizi zinamtisha na anawataka wafanye marekebisho mbalimbali katika idara wanazosimamia kabla ya kufanyiwa ukaguzi. Aidha kichwa kinamuuma usiku kucha na anashindwa kupata lepe la usingizi baada ya kumkaribisha Ghlestakovu kwake akidhania kuwa ndiye Mkaguzi Mkuu.

Viongozi wote wawili ni wenye kiburi. Mstahiki Meya anawazungumzia wawakilishi wa wafanyikazi Medi, Beka na Tatu kwa kiburi. Anawataka wawasilishe malalamiko yao upesi kwa kuwa hana muda wa kupoteza. Ana mambo muhimu ambayo anataka kushughulikia. Hataki kupoteza muda kufanya mazungumzo na wawakilishi wasiokuwa na lolote la maana la kumwambia. Anajipiga kifua na kusema kuwa uongozi wake hauwezi kulinganishwa na uongozi wa kiongozi yeyote na kama kungekuwa vyeti katika uongozi angekuwa na PhD. Aidha, anasema kuwa wananchi watamchagua tu hata mara ya nne, ya tano na hata ya sita akitaka. Isitoshe, Siki anapomtembelea kwake akiwa na nia ya kuwasilisha matatizo yanayowakumba wafanyikazi na kumwamkua kwa kumwita jina lake, Meya anakasirika. Anataka kuitwa Mstahiki Meya hata akiwa nyumbani kwake na nduguye. Mkuu wa Wilaya naye anaanza kuringa baada ya bintiye kuposwa na "Mkaguzi Mkuu". Anawaita wafanyibiashara kwake anawashutumu, anawakemea na kuwatusi na kupanga kuwadhalilisha zaidi. Aidha anawataka watayarishe zawadi nono nono za kumpa bintiye wakati wa arusi. Zaidi ya hayo, anawaeleza kwa kiburi kuwa hivi karibuni atakuwa baba mkwe wa Mkaguzi Mkuu na kuwataka askari kuwatangazia watu sokoni kuhusu habari hizi.

Zaidi ya hayo, Mstahiki Meya na Mkuu wa Wilaya hawadhihirishi kuwa na busara. Mstahiki Meya anashindwa kung'amua kuwa Bili hajali maslahi ya Baraza la mji wa Cheneo. Bili anampatia ushauri wa kupotosha na unaolengwa kumnufaisha yeye mwenyewe. Anamhadaa kuuza fimbo ya Meya na kumshauri kufanya *gentlemen's agreement* na mwanakandarasi. Aidha anamshauri kutosikiliza kilio cha wafanyikazi. Wakati ambapo mambo yanaenda mrama, Mstahiki Meya anamtafuta Bili asipatikane. Aidha anawaamini sana Diwani I na Diwani II. Maamuzi anayofanya kwa kuzingatia ushauri wao yanamtia matatani. Mwishowe anajuta kutoweza kutambua kuwa hawa aliowategemea katika maamuzi muhimu walikuwa wanamdanganya.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya naye amekosa busara. Ghlestakovu ameweza kumdanganya kwa urahisi kuwa yeye ni ofisa mwenye cheo kikubwa huko Pitasbag.

Aidha, anatumia muda na fedha nyingi kumstarehesha mtu ambaye hana ithibati kamili kuwa ndiye Mkaguzi Mkuu. Isitoshe, Mkuu wa Wilaya mwenyewe anakubali kuwa amekuwa juha. Anatueleza ya kwamba amewahi kuwalaghai majangili na majambazi ambao wangeweza kuiba dunia mzima. Anashangaa ni vipi kijana mdogo anaweza kumlaghai.

Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya ni walafi. Mkuu wa Wilaya anapotembelea maduka ya wafanyibiashara, anachukua matunda yaliyooza na kuyabugia. Matunda ambayo hata wasaidizi wa pale madukani hawawezi kuyala. Mstahiki Meya naye ni mlafi. Dida ambaye ni mtumishi wake wa nyumbani anapomwandalia kiamsha kinywa cha chai kwa mayai, analalamika kwamba mayai ni madogo. Anachukua yai moja na kulibwakia harakaharaka. Anakabwa na yai kooni kisha anapiga funda moja la chai moto ambayo inamchoma. Waandishi wote wawili wanadhihaki wahusika wao wakuu kwa ulafi wao. Mtindo huu wa dhihaka unatekelezwa kwa upigaji chuku kuhusu ulafi wao.

Zaidi ya hayo, viongozi wote wawili ni wabadhirifu. Mkuu wa Wilaya anatumia fedha na mali ya serikali kumtembeza Ghlestakovu kuzuru kitengo cha matibabu na cha elimu pia anamlipia nauli ya safari ya kwenda kumwona mjomba wake. Mstahiki Meya naye amepanga kuwapa mameya ambao wanakuja kuzuru mji wa Cheneo makaribisho kabambe. Amepanga kuwapa vyakula kutoka tamaduni zote aidha amepanga kuagiza mvinyo na divai kutoka ng’ambo huku Baraza la mji likiwa halina pesa za kumudu mahitaji ya kimsingi kama vile kulipa mishahara ya wafanyikazi na kununua vifaa vya utendakazi. Isitoshe, anakopa mikopo kwa wafadhili ambayo Baraza haliwezi kulipa na ambayo itabidi wajukuu na vitukuu vyao kulipia kwa riba.

Kwa jumla, wahusika hawa wawili wanaingiliana kwa kiasi kikubwa. Waandishi wa tamthilia hizi wanalandana katika kuwasawiri.

### 4.2.2 Diwani II na Bw. Huruma

Diwani II ni kiongozi anayesimamia kitengo cha uhusiano mwema katika *Mstahiki Meya*. Naye Bw. Huruma ni kiongozi anayesimamia kitengo cha afya na matibabu katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*. Wote wamekosa uwajibikaji. Bw. Huruma amemwajiri Heibna ambaye hawezi kuwasiliana na wagonjwa kwani hajui neno hata moja la Kirusi. Hospitali ni chafu. Malazi na mavazi ya wagonjwa ni machafu mno. Wagonjwa hawapatiwi tiba yoyote kwa kuwa ni watu wa tabaka la chini. Aidha, wagonjwa

wanafukuzwa kutoka hospitali kabla ya kupata nafuu.

Kwa upande mwingine, Diwani I1 naye amekosa uwajibikaji. Anamdanganya na kumpotosha Meya licha ya kuunga mkono pendekezo la kujiongezea mishahara bila kujali kuwa Baraza lilikuwa na mahitaji mengi na muhimu ya kifedha. Isitoshe, anataka kulipwa marupurupu baada ya kuketi katika mkutano na kupanga njama ya kuuza fimbo ya Meya.

Aidha, Diwani II na Bw. Huruma ni wanafiki. Bw. Huruma anawafukuza wagonjwa kutoka hospitalini kabla ya kupata nafuu kisha anamweleza Ghlestakovu kuwa wagonjwa ni wachache mno katika hospitali kwa sababu ya usimamizi bora, usafi na matibabu mazuri wanayopata. Anajifanya rafiki mwaminifu kwa Bw. Hakimu, mratibu wa Elimu na Bw. Posta lakini anapoingia chumbani kumwona Ghlestakovu, anawasengenya na kuwashutumu vikali. Anamweleza Ghlestakovu kuwa Bw. Hakimu ana uhusiano wa kimapenzi na mke wa Dob na kwamba Bw. Posta anachelewesha barua za wateja wake na kumhusu Mratibu wa Elimu anamweleza kuwa anapanda mawazo maovu katika akili za vijana. Habari anazotoa zingalikuwa na athari kubwa kwa viongozi hawa kama Ghlestakovu angalikuwa Mkaguzi Mkuu. Fauka ya hayo, anakwenda kwa Mkuu wa Wilaya kumpongeza kwa kuposwa kwa bintiye ingawa anamchukia, kumbeza na kumwona kama mtu duni asiyestahili uongozi.

Mbali na hayo, Diwani II na Bw. Huruma ni wafisadi. Diwani II anaunga mkono njama ya kulifisidi Baraza zaidi kwa kuiba fimbo ya Meya na kuiuza ng'ambo pia anataka kulipwa ovataimu na marupurupu baada ya kuketi katika mkutano wa kupanga jinsi ya kuiba fimbo ya Meya. Bw. Huruma naye akimdhania Ghlestakovu kuwa Mkuu wa Wilaya anamhonga shilingi mia nne ili asifanye ukaguzi katika idara anayosimamia.

Hali kadhalika, viongozi wote ni wenye tamaa na ubinafsi. Bw. Huruma anachelea kupoteza ajira yake. Anapopata habari za kuwasili kwa Mkaguzi Mkuu anaamka mapema kwenda kumhonga. Naye Diwani II ni mwenye sifa iyo hiyo. Anaunga mkono mawazo ya Bili na ya Diwani I ya kuuza fimbo ya Meya aidha anataka madiwani wapatiwe nyongeza ya mishahara. Isitoshe, anaridhia wazo la Meya la kutowatoza madiwani kodi.

### 4.2.3 Diwani I na Bw. Hakimu

Diwani I ni kiongozi anayesimamia swala la usalama katika wadi. Naye Bw. Hakimu anasimamia mahakama ya mji. Waandishi Gogol na Arege wamewasawiri wahusika

hawa kwa njia inayoshabihiana. Ni wafisadi, wasiowajibika na wanaotumia mamlaka yao vibaya. Hakimu anapokea hongo ya vijibwa kutoka kwa watuhumiwa. Aidha, ana mpango wa kujinufaisha kutokana na kesi inayowakabili cheptovichi na Valinski. Amepanga kulipeleka jibwa lake kuwinda katika bustani ya Cheptovichi siku moja na katika bustani ya Valinski siku ya pili. Isitoshe, anamhonga Ghlestakovu shilingi mia nne.

Kwa upande mwingine, Diwani I ni mfisadi. Anakubali fimbo ya Meya iuzwe ili waweze kujipatia malipo zaidi. Aidha, anamwomba Meya kutumia mamlaka aliyo nayo kuunda kamati za madiwani ili wawaunge mkono. Anafahamu kwamba Baraza halihitaji kamati hizi kwani hazitaleta manufaa yoyote kwa Baraza.

Aidha, wote wawili ni wenye ubinafsi na tamaa. Bw. Hakimu anapokea hongo kutoka kwa watuhumiwa pia anatoa hongo kwa Ghlestakovu kwani hataki kupoteza kazi yake. Diwani I naye anadai ovataimu kwake na Diwani II pamoja na malipo ya Bili kwa kutoa ushauri. Ukweli ni kwamba hakuna haja ya malipo haya kwani mkutano waliokuwa nao ni wa kupanga njama za kujidumisha mamlakani. Kadhalika, anakubaliana na hoja ya kuuzwa kwa fimbo ya Meya ili kujipatia hela. Anasema haoni haja ya kupinga kwani fimbo ni yao na Baraza ni lao pia. Anasema kuwa madiwani hawamudu kuvaa nguo nzuri na kuwa nadhifu kama wenzao katika mapokezi ya mameya wanaokuja kutoka nga’mbo. Isitoshe, anaunga mkono pendekezo la kujiongeza mishahara bila kujali kuwa Baraza lilikuwa na mahitaji mengi na muhimu ya kifedha.

Hali kadhalika, viongozi wote wawili wamekosa uwajibikaji. Diwani I anapaswa kuwahakikishia raia usalama lakini yeye ndiye anayewatuma polisi kuwachapa na kuwatupia vitoa machozi wanapogoma. Pia anatumia propaganda kuamsha uzalendo wa vijana kwa kupendekeza kuandaliwa kwa tamasha ya vijana kushindania tunu. Tamasha hizi zitapeperushwa kupitia vyombo vya habari.

Kwa upande mwingine, Bw. Hakimu naye hajawajibika. Mahakama anayosimamia ni chafu. Ofisi zake zimejaa kila aina ya takataka. Ngozi zilizotundikwa ili zikauke, mijeredi na vifaa vingine vya kuwindia vimechanganyikana ovyo na karatasi. Aidha, anamruhusu karani wake kugeuza ofisi za mahakama na kuzifanya kuwa vibanda vya kufugia kuku, bata na ndege. Karani wake ni mlevi na isitoshe anakiri mwenyewe kuwa maamuzi anayotoa kuhusiana na kesi za watuhumiwa si ya haki. Anasema:

> **Hakimu** …Nimekuwa nikikalia kiti cha hakimu hapa kwa muda wa miaka kumi na mitano, na kama ningepaswa kuzichunguza kumbukumbu za mahakama … Naam, najiosha mikono yangu! Solomoni mwenyewe hangejua vipi kutofautisha ukweli na uongo! (uk. 11)

Isitoshe, Bw. Hakimu hatilii maanani maslahi ya wafungwa. Hawajapatiwa chakula kwa muda wa majuma mawili.

### 4.2.4 Dida naYosif

Dida ni mfanyikazi wa nyumbani kwa Mstahiki Meya naye Yosif ni mtumishi wa Ghlestakovu. Wote ni wanyenyekevu na watiifu. Mstahiki Meya anapokabwa na yai kisha kuchomwa na chai, Dida anamwomba msamaha na kumpangusa. Aidha, anapoamrishwa amwachishe kazi mwenye kuleta mayai kwa madai kuwa ni madogo, hapingi anatii agizo hilo bila kuuliza maswali.

Kwa upande mwingine, Yosif ni mtumishi mwaminifu kwa mwajiri wake. Anamwagizia chakula hotelini, anakomdishia nyumba na zaidi ya hayo anakubali kuandamana naye kokote aendako.

Isitoshe, watumishi wote ni wenye busara. Dida anafahamu kuwa duniani kuna watu na viatu. Watu ni matajiri na viatu ni wananchi wa kawaida hasa wafanyikazi ambao wanateswa na kufinyiliwa kiuchumi na uongozi duni wa mji wa Cheneo. Mstahiki Meya anathamini watu wake mno. Hataki wadhurike. Anampeleka mke kujifungulia ng’ambo na hata watoto wake wanasomea huko. Yosif naye ni mwerevu. Anapogundua kuwa Mkuu wa Wilaya amekosea na kumdhania Ghlestakovu kuwa mtu mwingine, anaona hatari inayowakabili na anamshauri waondoke ili wasije wakajipata mashakani.

Zaidi ya hayo, watumishi wote ni wavumilivu. Dida anavumilia matusi na madhila kutoka kwa mwajiri wake. Mstahiki Meya anamdhalilisha na kumtusi. Anamlaumu baada ya kuchomwa chai. Anapoomba msamaha kwa makosa ambayo si yake, Meya hataki kumsikiliza. Naye Yosif anavumilia madhila anayotendewa na Ghlestakovu. Bwana wake si mtu wa kutunza fedha. Ni miezi miwili tangu watoke Pitasbag. Wako safarini kuelekea Saratovu. Wamekwama mjini kwa kuwa Ghlestakovu amemaliza fedha kwa kucheza kamari, kulipa nauli na kwa kukodi vyumba vya bei ghali kwa malazi wanapokuwa safarini. Isitoshe, Anavumilia njaa. Mpishi wa hoteli amekataa kuwapa

chakula kwa kuwa wamelimbikiza deni pale hotelini.

### 4.2.5 Askari

Hawa ni walinda usalama. Ni wahusika wakatili wasiokuwa na utu. Askari wa Baraza la mji wanavuruga mikutano ya wafanyikazi kwa kutumia nguvu zilizopita kiasi. Badala ya kutibua mikutano ile kwa njia ya amani, wanawafyatulia wafanyikazi risasi, kuwatupia vitoa machozi, kuwamwagia maji na kuwapiga kwa marungu. Askari katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* pia wana mwenendo uo huo. Wanawapiga na kubomoa vibanda vya wafanyibiashara wanaotoa malalamiko dhidi ya Mkuu wa Wilaya licha ya kuwalisha kauzu za chumvi.

Aidha, wamekosa uwajibikaji. Wanatekeleza yote wanayotaka mabwana wao bila kujali matokeo ya vitendo vyao vya kikatili. Polisi katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ni walevi. Prohorovu hawezi kushika zamu kwa sababu ni mlevi chakari. Mbali na hayo, wao hupokea hongo kutoka kwa wafanyibiashara na kukimbiakimbia ovyo mitaani wakiwa nusu uchi kwa kuwa hawapendi kuvaa mashati na suruali. Polisi katika *Mstahiki Meya* nao wanawadhulumu raia wanaopigania haki zao.

Polisi hawa pia ni watiifu. Mkuu wa Wilaya anapowaamrisha wawapige wafanyibiashara wanaomchukiza, wanafanya hivyo bila kuuliza maswali. Wanampiga mke wa Sajeni makalioni kwa tuhuma za kuzua rabsha sokoni mpaka anashindwa kuketi kwa muda wa majuma mawili. Wanatii amri ya Mstahiki Meya ya kuwapiga na kuwafurusha wafanyikazi wanaogoma. Aidha, polisi hawa wanapotumwa na makao makuu kwenda kuwakamata Mstahiki Meya, Diwani I na Diwani II wanafuata maagizo bila kuwa na woga kuwa wanakwenda kumkamata Meya wa Baraza la mji. Polisi wanatekeleza haya yote kwa kuwa wanataka kujidumisha kazini. Wanasahau kuwa kwa kutii maagizo yote yanayotolewa na wakuu wao, wanakuwa wanasaliti raia ambao wanawahakikishia ajira kwa kodi wanazotoa.

### 4.2.6 Dhiki ya wafanyikazi na wafanyibiashara

Wafanyikazi wa Baraza la mji wa Cheneo na wafanyibiashara wamedhulumiwa. Mstahiki Meya anawalipa wafanyikazi mishahara duni na inayocheleweshwa na wakati mwingine wanalipwa mishahara nusu. Wanapogoma ili kudai nyongeza ya mishahara, wanapigwa na kufyatuliwa risasi licha ya kutupiwa vitoa machozi. Meya amewatelekeza katika umaskini mkubwa. Hawawezi kumudu mahitaji ya kimsingi kama vile chakula, mavazi,

matibabu na elimu. Wafanyikazi wanakula mabaki ya chakula, chakula cha mbwa, mizizi na matunda ya mwitu. Mamake Dadavuo Kaole anampa mtoto mabaki yaliyolala. Hawezi kuyatokosa kwani hana pesa za kununulia mafuta au makaa. Wafanyikazi hawana pesa za kugharamia matibabu. Watoto wao wanafia mikononi mwao. Mtoto wa Kerekecha anafia mikononi mwake. Isitoshe, watoto wao wanafukuzwa shuleni kwa kukosa karo. Mbali na kushindwa kujikimu kimaisha, wanafanya kazi katika mazingira duni. Hawana vifaa muhimu vya utendakazi. Tunaelezwa kuwa wanasafisha vyoo bila glavu.

Kwa upande mwingine, wafanyibiashara wanapitia matatizo chungu nzima. Wanapokataa kumpa Mkuu wa Wilaya zawadi na kutoa malalamiko dhidi yake, anawatusi na kuwatumia askari ambao wanawapiga na kuwatusi. Anafunga maduka yao bila sababu maalum. Isitoshe, anachukua bidhaa kutoka madukani mwao bila kutoa malipo.

### 4.2.7 Ghlestakovu na Bili

Ghlestakovu na Bili ni wahusika wengine ambao wanalandana kabisa. Wote ni wadanganyifu. Ghlestakovu anamdanganya Mkuu wa Wilaya baada ya kugundua kuwa amemdhania kuwa mtu mwenye cheo kutoka Pitasbag. Anajifanya kuwa mtu mashuhuri aliye na uwezo wa kutangamana na mawaziri na mabalozi kutoka nje ya nchi aidha anajifanya kuwa mwandishi wa michezo ya tamthilia. Isitoshe, anajifanya kumposa bintiye Mkuu wa Wilaya. Zaidi ya hayo, anawalaghai Mkuu wa Wilaya, Bw. Hakimu, Mratibu wa Elimu na Bw. Huruma shillingi mia nne kutoka kwa kila mmoja aidha anajipatia mikopo zaidi kutoka kwa Dobchinski, Bobchinski na wafanyibiashara. Baada ya kuwachezea shere na kujipatia fedha nyingi, anatoweka asirudi.

Kwa upande mwingine, Bili naye ni mdanganyifu. Anampemdekezea Mstahiki Meya kuiuza fimbo ya Meya ng'ambo. Anapanga mpango kabambe wa namna wataiiba kutoka pale ofisini. Baada ya Meya kufanya yote ambayo anashauriwa na Bili, mambo yanatumbukia nyongo pale ambapo anatambua kuwa wageni karibu wanafika na wafanyikazi hawajarejea kazini na kwamba hawawezi kupata watu wa kuchukua nafasi za wafanyikazi. Hapo ndipo anapogundua kwamba alidanganywa na kwamba Bili amekwenda mafichoni. Alichotaka kutoka kwa Mstahiki Meya ni pesa ambazo tayari amepata.

Wahusika wote wanapenda makuu. Ghlestakovu ni mfanyikazi wa cheo cha chini katika utumishi wa serikali lakini anapokuwa safarini kwenda kumzuru babake katika mkoa wa

Saratovu, anataka kula vyakula vya bei ghali, kulala katika hoteli za kifahari aidha anataka kuketi katika viti maalum anaposafiri. Bili naye anajifanya kuwa mshauri mkuu wa Mstahiki Meya wakati yeye si diwani, anatamani kumpeleka mkewe ng'ambo akajifungue. Aidha, anataka watoto wake wakasome ng'ambo. Isitoshe, anataka kustarehe katika mahoteli ya kifahari.

Zaidi ya hayo, wote wana tamaa ya pesa. Ghlestakovu anatamani kuishi maisha ya kifahari aidha ana tamaa ya pesa. Tamaa inayompelekea kuchukua hongo kutoka kwa viongozi wanaomdhania kuwa Mkaguzi Mkuu kutoka Pitasbag.

Kwa upande huo mwingine, Bili naye ana tamaa kubwa ya pesa na utajiri. Hulka hii inamfanya kujifanya rafiki wa Mstahiki Meya lakini anachotaka ni fursa ya kumpotosha ili ajinufaishe kifedha. Ushauri wake kwa Meya kuwa amwache mwanakandarasi aende kortini ili Baraza limlipe hasara baada ya mkataba wake kusimamishwa, ulilenga pale pale pa kujinufaisha kifedha. Anamwambia Meya kuwa jina kuharibika si kitu, kwamba kilicho muhimu ni tumbo. Isitoshe, anamwambia Meya asimsahau atakapopatiwa fungu lake na mwanakandarasi.

### 4.3 Mandhari

Tamthilia za waandishi Gogol na Arege zinaingiliana kimandhari. Maelezo yao kuhusu mazingira ya utendaji katika tamthilia hizi mbili yanazidi kushadidia nadharia tete yetu kuwa, matini za kifasihi huchangizana na kuingiliana. Katika tamthilia tumesawiriwa mandhari sawa ya kijamii.

Tamthilia hizi zinaegemezwa kwa kiasi kikubwa katika mandhari ya zahanatini, nyumbani na ofisini. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* tunakumbana na mandhari ya zahanatini. Tunakutana na Siki na Waridi ambao wanawahudumia wagonjwa. Wagonjwa ambao wamefika kupata matibabu ni wengi mno lakini tunaelezwa kuwa hakuna dawa na zilizopo ni *painkillers* tu. Mamake Dadavuo Kaole anamleta mtoto anayeendesha tumbo kwa kula wali na maharagwe yaliyolala.

Kwa upande mwingine, hospitali katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ni chafu. Wagonjwa ni wengi mno mavazi na malazi ya wagonjwa ni machafu. Daktari Heibna hawezi kuwatibu wagonjwa kwani hawezi kuzungumza neno moja la Kirusi. Wagonjwa hawatibiwi. Wanapatiwa matibabu ya kiasili. Daktari hajali kama watakufa au kama watapona kwa kuwa wagonjwa hawa ni tabaka la chini. Mandhari ya zahanati

yanaonyesha hali duni inayokumba taasisi za umma.

Aidha, tunasawiriwa mazingira ya ofisini. Mipango mingi inatekelezwa ofisini. Katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* tunakutana na Mstahiki Meya na Madiwani wakiweka mikakati ya jinsi ya kuendelea kujidumisha mamlakani. Kadhalika, Meya amefika ofisini mapema kushughulikia mpango wa kuwakaribisha mameya ambao wanakuja kuzuru Baraza la mji wa Cheneo. Ni mumu humu ambamo anazua mpango wa kumtimua mwanakandarasi. Isitoshe, Mstahiki Meya amemwalika Mhuburi ofisini mwake kwa kuwa anataka kuombewa ili aweze kudumisha uongozi wake. Maombi yao yanafanyika kwa sauti ya juu kiasi cha kuwashtua askari ambao wanadhani kuwa Mstahiki Meya amevamiwa na wafanyikazi. Askari wanaingia na kuwaamrisha watu wote walale chini. Baadaye wanabaini kwamba ni maombi yanayoendelea. Mbali na hayo, Mstahiki Meya anamwalika Diwani III ofisini mwake ambapo anamwagiza kuongeza mishahara ya madiwani. Kwingineko, tunakutana na Meya, Bili, Diwani I na Diwani II katika ofisi ta Meya wakipanga njama ya jinsi ya kuiba fimbo ya Meya.

Kwa upande mwingine, Mkuu wa Wilaya anawaita ofisini mwake maofisa wanaosimamaia idara mbalimbali katika mkutano wa dharura ili kujadili athari za habari ambazo zimemfikia kuhusu kuwasili kwa Mkaguzi Mkuu.

Mbali na hayo, tumesawiriwa mandhari ya nyumbani kwa Meya. Mna makochi makubwa makubwa, mazulia yanayopendeza vilevile kuna vyakula vya aina mbalimbali. Meya ni mlafi analalamikia udogo wa mayai wakati ambapo wananchi wake hawana chakula. Wanakula mizizi na matunda ya mwitu. Aidha, Siki anafika nyumbani kumzuru nduguye Meya. Anataka kumweleza matatizo yanayowakumba wafanyikazi. Anamtahadharisha dhidi ya kuridhia maamuzi ya watu wachache bila kuwashirikisha raia waliomchagua. Ushauri wa Siki unamkasirisha Meya ambaye anamwamuru Gedi kumwondoa pale na kuhakikisha kwamba harudi hapo tena. Naye Mkuu wa Wilaya anamkaribisha Ghlestakovu kwake na kumpa chumba kimoja ambacho anakitumia kama ofisi kushughulikia maslahi ya wateja ambao wamekuja kumzuru ili kumhonga na wengine wameleta malalamiko yao dhidi ya Mkuu wa Wilaya.

### 4.4 Hitimisho

Katika sura hii, tumeendendeleza mjadala wetu kuhusu mwingilianomatini kati ya tamthilia zilizoteuliwa. Kwa mifano anuwai, tumefafanua jinsi tamthilia hizi mbili

zinavyoingiliana na kuchangizana kiwahusika. Wahusika Mkuu wa Wilaya wa *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na Mstahiki Meya wa *Mstahiki Meya* wanashabihiana. Wote ni viongozi wafisadi, wakatili, wadanganyifu, wanafiki, wenye ubinafsi na tamaa, waoga, wasiowajibika na wanaotumia mamlaka yao vibaya. Mstahiki Meya anawadhulumu wafanyikazi jinsi anavyopenda. Hataki kusikiliza manung'uniko yao. Anatumia mbinu mbalimbali kujidumisha mamlakani. Mkuu wa Wilaya naye anatumia mamlaka aliyopewa kukandamiza umma.

Mbali na wahusika hawa wakuu, tumehakiki mwingiliano kati ya maofisa wanaosimamia idara mbalimbali. Tumeonyesha namna Diwani I na Bw. Hakimu wanavyodhihirisha mwingiliano wa kiwango cha juu. Wote wanaiga mienendo ya viongozi wao. Wamekosa uwajibikaji, wafisadi na wanatumia mamlaka waliyotwikwa vibaya. Aidha, Diwani II na Bw. Huruma wanaonyesha mwingiliano. Wanafuata nyayo za viongozi. Mbali na wahusika hao, tumedhihirisha mwingiliano kati ya Dida na Yosif ambao ni watumishi watiifu na wanyenyekevu. Aidha, tumeonyesha jinsi polisi katika tamthilia zote mbili wanavyoingiliana na kuchangizana. Wote ni wakatili. Wanawapiga wanyonge kwa marungu badala ya kuwapa usalama. Wametepetea katika kutekeleza majukumu yao. Wafanyikazi na wafanyibiashara ni wahusika wengine wanaodhihirisha mwingiliano. Wote ni wanyonge na wanakandamizwa na viongozi wao.

Ingawa wahusika hawa wanahitilafiana kwa njia moja au nyingine, uhusiano wao unatudhihirishia kuwa swala la wahusika kuingiliana ni halisi. Nikolai Gogol na Timothy Arege waliandika katika vipindi na mazingira tofauti lakini kazi zao zinaingiliana kimatini. Huku kuingiliana hakumaanishi kuwa waandishi huiba mawazo kutoka kazi za waandishi waliowatangulia. La, kazi za kisanaa huingiliana kwa kuwa fasihi ni zao la jamii na waandishi huchota malighafi yao kutoka jamii.

Aidha, tumehakiki jinsi tamthilia hizi zinavyoingiliana kimandhari. Tumedhihirisha jinsi waandishi Gogol na Arege wametusawiria mazingira ya kijamii yanayofanana. Mazingira haya ni ya zahanatini ambapo wagonjwa wanafika kutafuta matibabu, ya ofisini ambamo mipango mingi ya uongozi inatekelezwa na ya nyumbani wanamoishi Mstahiki Meya na Mkuu wa Wilaya pamoja na familia zao. Mna makochi na mapambo ya kila aina kinyume na maskini ambao wanaishi kwenye mabanda. Mandhari wanamoishi Meya na Mkuu wa Wilaya yanawasawiri kama watu walio na chao.

# SURA YA TANO

# MWINGILIANO WA KIMAUDHUI

## 5.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumehakiki maudhui kama kipengele cha kimwingilianomatini. Kama tulivyoeleza katika sura ya pili, maudhui ni mawazo mbalimbali yanayoibuka katika kazi ya fasihi na dhamira ni swala kuu linalojitokeza katika kazi ya kifasihi kuanzia mwanzo hadi mwisho wa kazi hiyo. Hujengwa na kuathiri vipengele vingine vyote vya kazi husika maksudi ili kujenga dhamira. Mathalan maudhui, wahusika, lugha na vipengele vya kimuundo huteuliwa ili kuibua dhamira maalum.

Julia Kresteva anasisitiza kuwa, hamna matini yoyote ile ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake. Kazi za kifasihi huingiliana na kuchangizana katika kipengele kimoja au zaidi. Waandishi wa kifasihi wanapoandika kazi zao, hawana budi kuwa na mshabaha katika maswala wanayozungumzia. Hii ni kwa sababu fasihi ni zao la jamii na wote huchota malighafi yao kutokana na jamii. Isitoshe, binadamu wote ulimwenguni hughasiwa na maswala yanayofanana. Kwa sababu hii, si ajabu kupata waandishi waliokulia katika mazingira mbalimbali wakiandika mambo yayo hayo kwa njia zinazolandana.

Bakhtin (1990) anasema kuwa semi zote kimaumbile ni za kisemezano. Kwa mujibu wa maoni ya mwananadharia huyu, tumehakiki jinsi tamthilia hizi zinavyoingiliana kimaudhui. Waandishi Gogol na Arege wameangazia mambo mengi wanayoyaona katika jamii zao. Baadhi ya mambo hayo ni uongozi dhalimu, ufisadi, ukosefu wa uwajibikaji, unafiki, uchafuzi wa mazingira, migogoro, utabaka na kadhalika.

## 5.2 Uongozi mbaya

Kwa mujibu wa nadharia ya Mwingilianomatini, matini tofauti huingiliana katika kuzungumzia maswala anuwai yanayojitokeza katika jamii. Mathalani tamthilia hizi mbili *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* zinashadidia kauli hii kwa kuingiliana katika kushughulikia swala la uongozi mbaya. Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya ndio viongozi wenye vyeo vya juu zaidi mjini. Wote wawili wameshindwa kutekeleza wajibu wao ipasavyo. Wanapaswa kulinda mali ya wananchi na kuwahakikishia raia usalama lakini hawafanyi lolote.

Uongozi wa miji yote miwili umejaa viongozi wenye ubinafsi, ukatili, uongo, tamaa na ushauri potovu, wafisadi, waliokosa busara na wasiojali maslahi ya wengine. Hali hii inapelekea kudorora kwa miundo msingi na huduma za umma kwa jumla. Mkuu wa Wilaya ni kiongozi mbinafsi, katili na mwenye kuwahangaisha na kuwakandamiza raia. Anawashurutisha wafanyibiashara kumpa zawadi za nguo wakati wa siku kuu ya pasaka, siku kuu ya Mtakatifu Antonio na Mtakatifu Basili. Aidha anatoa amri kwa askari kuwapiga, kuwavuta ndevu na kuwalisha chumvi wafanyibiashara ambao wanatoa manung'uniko dhidi yake. Isitoshe, anachukua bidhaa kutoka maduka yao bila kutoa malipo. Mfanyibiashara mmoja analalamika:

> **M/BIASHARA 2**: Anakuja na kutwaa chochote "Ahaaa, ndugu yangu, una nguo nzuri sana! Itume nyumbani kwangu" inatubidi tuitume, na inaweza kuwa jora nzima ya meta 40!" (Uk. 55)

Kwa upande mwingine, Mstahiki Meya naye ni kiongozi mbinafsi, mkatili na mwenye kuwakandamiza wafanyikazi wake kwa hasira, dharau na ukali. Kwa mfano Gedi anatakiwa kupiga saluti kila anapoingia na kutoka kwa Mstahiki Meya. Dida ambaye ni mfanyikazi wa Meya anakiri kuwa kazi yake ya kufagia ni ya kudhalilishwa kwa matusi kutoka kwa bwana Meya. Kiongozi mzuri ni yule anayeshirikiana na wenzake na mwenye kujali maslahi ya wengine. Meya hataki kusikiliza matakwa na kilio cha wafanyikazi. Anawalipa wafanyikazi wa Baraza mishahara duni na wanapogoma kulalamikia kupatiwa nyongeza ya mishahara, anatoa amri kwa polisi ambao wanawafurusha kwa kuwapiga na kuwatupia vitoa machozi.

Uongozi mbaya wa Meya pia unadhihirika pale anapokutana na baraza la madiwani ili kujadiliana kuhusu namna ya kuwakomesha watu ambao walikuwa wakidai haki yao. Katika mkutano anawakumbusha madiwani wenzake kuwa hangetaka askari wake kuwaua wananchi mara hii. Hii ni ishara tosha kuwa askari wake walikuwa wakitumia ukatili kwa kiwango cha kuwaua wananchi. Unafiki unajitokeza anapoeleza kuwa, huu ulikuwa mwaka wa uchaguzi na watu wakifa wakati kama huu angeweza kupoteza kura kwa kiwango kikubwa. Isitoshe, Meya anatenga fedha nyingi za kufadhili mapokezi ya wageni ambao wangezuru nchi yake. Anachukua hatua hiyo akionekana kutotilia maanani matatizo ambayo yalikuwa yakiwakumba wanacheneo. Anasema:

**Meya**: …Hoteli ya kifahari, vyakula kutoka kila tamaduni duniani. Si sima la hasha! Mvinyo nitauagizia kutoka Urusi na divai kutoka Ufaransa... (Uk. 25)

Aidha, viongozi wowote wawili wanaendeleza wizi wa mali ya umma badala ya kuupinga. Mkaguzi Mkuu amepora pesa zilizotolewa kujenga kanisa la hospitali. Aidha anachukua hongo kutoka raia maskini.

Kwa upande mwingine, Mstahiki Meya naye baada ya kuchaguliwa na kushika usukani anatafuta mianya ya kumwezesha kujilimbikizia mali. Anaufisidi umma kwa kujigawia viwanja vinane na kumgawia vingine Bili. Aidha, Meya, Bili, Diwani I na Diwani II wanapanga njama ya kuiba fimbo ya Meya. Diwani I aitoe yeye ofisini kisha baada ya wiki atangaze kuwa fimbo iliibiwa kufuatia rabsha zilizotokea na kwamba uchunguzi umeanzishwa. Isitoshe, tunaelezwa kuwa anawahonga askari kwa kuwapatia asilimia ishirini ya nyongeza ya mshahara ili waendelee kuunga mkono uongozi wake.

Mbali na hayo, viongozi Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya wanatumia mbinu hasi za utawala. Mkuu wa Wilaya anatumia hongo, vitisho, polisi na mbinu ya tenga-utawale. Anatishia kufunga maduka ya wafanyibiashara ambao wanatoa manung'uniko dhidi yake aidha amepanga kuwahonga askari ili wakubali kuonyesha kuridhika kwao mbele ya Mkaguzi Mkuu. Zaidi ya hayo, anatumia askari kuwanyamazisha wafanyibiashara wanaolalamika dhidi yake.

Kwa upande mwingine, Mstahiki Meya naye anatumia mbinu zizo hizo. Anatumia propaganda, vitisho na vishawishi kuwadhibiti raia. Anawadanganya Daktari Siki na Waridi kwamba shehena ya dawa iko njiani, imeagizwa ili kuonekana kwamba Baraza limewajibika. Jambo hili linasababisha mateso na hata maafa katika zahanati kwa kukosa dawa. Pia anamtaka kinara wa uhusiano mwema na mawasiliano kuitaka idhaa ya Baraza kucheza nyimbo za kizalendo ili watu waridhike nyoyo licha ya hali duni ya maisha inayowakabili. Zaidi ya hayo, Diwani I anataka kuwaambia watu kuhusu kujitolea kwa Baraza la Cheneo kutetea demokrasia na hasa uhuru wa kujieleza. Hii ni propaganda inayonuiwa kuwasadikisha raia kuwa maisha yao yanatiliwa maanani. Hali kadhalika, anakubali kuundwa kwa kamati za madiwani. Kufuatia hatua hii, madiwani wengi wangeweza kufanywa wakuu wa kamati hizo. Inapendekezwa kuwa ni madiwani ambao walikuwa wakimuunga mkono pekee ambao wangeteuliwa kusimamia kamati hizo. Kiundani, hiyo ilikuwa ni njia ya kuhakikisha kuwa Meya angeendelea kukwamilia mamlakani japo hali ya maisha ya watu aliokuwa anawaongoza iliendelea kuwa mbaya

siku baada ya siku. Isitoshe, anatumia askari kuwafurusha wafanyikazi wanaogoma kudai haki zao kwa kuwafyatulia risasi na kuwatupia vitoa machozi. Mbali na hayo, viongozi waadilifu wanatengwa. Meya anamtenga Diwani III kwa sababu anatetea haki za wafanyikazi na kupinga mapendekezo ya; kutotozwa kodi kwa mishahara ya madiwani na nyongeza ya mishahara na marupurupu kwa walinda usalama. Anamwambia Mstahiki Meya kuwa Baraza haliwezi kutosheleza haya kwani lina nakisi ya shilingi milioni mia moja ishirini. Kwa sababu hii, Meya anamchukia na kumtazama kama kibaraka.

Uongozi wa hospitali katika tamthilia zote ni mbaya. Bw. Huruma ambaye ni mkuu wa idara ya matibabu ametepetea katika kutekeleza wajibu wake. Hospitali ni chafu. Malazi na mavazi ya wagonjwa hayajasafishwa kwa muda mrefu. Licha ya wagonjwa waliolazwa kuwa wengi, hawatibiwi. Wanapatiwa matibabu ya kiasilia. Bw. Huruma anamruhusu Daktari Heibna kuendelea kuwashughulikia wagonjwa hata ingawa hajui hata neno moja la Kirusi.

Kwa upande mwingine, Uongozi wa Mstahiki Meya vilevile umeshindwa kukadiria mahitaji ya zahanati. Hamna hazina ya dawa kwenye zahanati, kilichobakia ni dawa za kudhibiti uchungu tu. Aidha, wagonjwa waliolazwa wanahitajika kulipia kitanda pasipo kupata matibabu. Waridi anasema: "Tukae tu na kungoja. Nao wasubiri. Wenye kulazwa nao walipie!" (uk.6).

Uongozi wa Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya umechangia uharibifu wa mazingira katika miji yote miwili. Viwango vya usafi vimedorora. Miji yote ni michafu na inanuka uvundo. Katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*, tunaelezwa kwamba walinzi hawajafagia barabara za mitaa kwa muda mrefu na kuna rundo la takataka karibu na ua ya mshona viatu. Mambo ni yayo hayo katika tamthilia ya *Mstahiki Meya*. Mji ni mchafu, haujafagiliwa kwa sababu ya migomo ya wafanyikazi. Safari ya wageni wanaokuja kuzuru mji wa Cheneo imeahirishwa kwa sababu ya uchafu na ukosefu wa maji safi. Viongozi wote wawili hawafanyi lolote kuhakikisha kuwa miji ni safi.

Elimu wanayopata vijana katika jamii zote mbili ni duni. Vijana waliohitimu hawawezi kutekeleza kazi katika taaluma walizosomea vyuoni. Tunaelezwa kuwa madaktari hawezi kufanya kazi zao vyema hata baada ya kuhitimu kutoka vyuo vikuu. Mstahiki Meya anampeleka mkewe ng'ambo kujifungua. Anasema kuwa madaktari wa Cheneo ni wa kutia wasiwasi. Kadhalika, amewapeleka watoto wake kusomea ng'ambo. Anadai kuwa elimu ya Cheneo ni ya viwango vya chini mno.

Kwa upande huo mwingine, vijana katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* hawapatiwi elimu bora. Mkuu wa Wilaya analalamika kuwa walimu wanapanda mawazo mabovu akilini mwa vijana. Isitoshe, walimu wana tabia ya ajabu. Wanakunja nyuso zao wanapofundisha.

### 5.3 Ukosefu wa uwajibikaji

Viongozi wote katika tamthilia za *Mstahiki Meya* na *Mkaguzi Mkuu* wa Serikali wamekosa uwajibikaji. Idara wanazosimamia zimejaa uozo. Wameshindwa kuwa kielelezo bora kwa viongozi wanaofanya kazi chini yao. Mkuu wa Wilaya hafanyi lolote kuhakikisha kuwa mji ni safi. Takataka zimerundikana karibu na ua ya mshona viatu. Mikokoteni arubaini haitaweza kuzoa rundo hilo la takataka. Barabara hazijafagiliwa. Mkuu wa Wilaya apatapo habari za kuwasili kwa Mkaguzi Mkuu, anawaamuru walinzi kufagia barabara zilizo karibu na hoteli. Isitoshe, anawaamuru polisi kuwachapa raia wasiokuwa na hatia. Mke wa Sajeni anachapwa na polisi mpaka anapata maumivu mabaya makalioni. Anashindwa kukalia kiti kwa muda wa majuma mawili.

Kwa upande mwingine, Mstahiki Meya hajaendesha mambo inavyopasa. Zahanati ya Baraza la mji haina dawa zilizopo ni *painkillers* tu. Jambo hili linasababisha hali ya kutoweza kukabiliana na idadi ya wagonjwa wanaohitaji matibabu. Wagonjwa ambao wamefika zahanatini kupata matibabu ni wengi mno. Wagonjwa wanafariki kwa kukosa matibabu. Maneno ya Daktari Siki yanadhihirisha hali mbaya inayowakumba wagonjwa. Anasema: “Kweli, ni jana tu kitoto kidogo kimenifia mikononi mwangu kwa njaa na ugonjwa…” (Uk. 12)

Meya hataki kubuni mikakati ya kukabiliana na hali duni ya kiuchumi. Anadai kuwa hakuna baraza lenye uthabiti kama lake, kwamba Cheneo ni kisiwa cha kupigiwa mfano. Aidha, hawazii gharama ya migomo ya wafanyikazi. Badala yake anapuuza na kusema kwamba watakaogoma watafutwa kazi na kuwaajiri vijana waliohitimu hivi karibuni kutoka vyuo vikuu. Matokeo ni kwamba viwango vya usafi mjini vinazorota hali ambayo inasababisha kuahirishwa kwa ziara ya wageni. Isitoshe, anakubali kutolewa maamuzi muhimu ya kiuongozi na Bili; mtu ambaye hana taaluma wala sifa ya uongozi.

Aidha, Mstahiki Meya hajabuni mikakati yoyote ya kuimarisha viwango vya elimu na matibabu. Anawepeleka watoto wake kusomea ng’ambo huku akidai kuwa elimu ya Cheneo ni ya kawaida mno. Amezorotesha hali ya utoaji wa huduma za afya ilhali

anatumia fedha za umma kumpeleka mkewe kuzalia ng'ambo kwa madai kuwa madaktari wa Cheneo ni wa kubabaisha tu.

Mstahiki Meya anafuja pesa za Baraza kwa kumlipa Mhubiri shilingi laki moja kila mwezi na kufidia gharama ya usafiri kila juma, anaidhinisha nyongeza ya mishahara kwa madiwani, anatumia *entertainment vote* kuwaburudisha na kuwastarehesha marafiki pamoja na familia zao. Amepanga kuagiza mvinyo na divai kutoka ng'ambo huku akijua kwamba Baraza halina uthabiti wa kifedha. Isitoshe, anaidhinisha uundaji wa kamati za madiwani bila kuwazia gharama yake. Anafahamu kwamba Baraza halihitaji kamati hizi ila anaidhinisha uundaji wake ili kujifaidi.

Aidha, Mstahiki Meya anapuuza malengo ya mji katika mpango wa kimaendeleo wa miaka kumi na kudai kuwa wana malengo ya kimaendeleo ya kimilenia. Upuuzaji huu unamfanya kutozingatia afya ya raia ambayo ni mojawapo ya mahitaji ya kimsingi ya raia. Meya anasema:

> **MEYA**: Hapa ni kwangu Siki. Usinifuate kwangu kunitusi. Mipango ya miaka kumi ni upuuzi. (kimya) Sisi tuna malengo ya kimaendeleo ya milenia. (Uk. 14)

Zaidi ya hayo, Meya anaidhinisha kulipwa kwa ovataimu kwa Diwani I, Diwani II na kulipwa kwa huduma ya ushauri kwa Bili kwa kushiriki tu katika kikao cha kubuni mikakati ya kuwanyamazisha wafanyikazi. Meya hawazii kuhusu athari za uongozi wake kwa kizazi cha kesho. Anasema kuwa wageni watakaokuja watawapa mikopo ya kulipia mishahara bila kuwaza kuwa mikopo hii itakuwa mzigo mzito kwa vizazi vya kesho kulipa.

Bw. Huruma, Bw. Hakimu, Mratibu wa Elimu, Bw. Posta, Diwani I na Diwani II na Mhubiri ni viongozi wengine ambao wanadhihirisha maudhui ya ukosefu wa uwajibikaji. Bw. Huruma hajishughulishi na maslahi ya wagonjwa kwa sababu ni wa kawaida mno. Vifo vya wagonjwa havimtishi, anasema:

> **BWANA HURUMA**: Oh! Daktari na mimi tumepanga kila kitu njia halisi za kitabibu. Kadri matibabu yako yanavyokuwa ya kawaida, ndivyo yanavyokuwa bora. Hatujishughulishi na madawa ya ghali. Wagonjwa wetu ni wa

> kawaida. kama wanakufa sawa, wanakufa! Kama wanapona, basi hupona! Na ingekuwa vigumu sawa Heibna kuzungumza nao. Ni daktari mzuri sana, lakini hajui hata neno moja la kirus(u.k 3)

Aidha, amemwajiri Heibna ambaye hana lugha ya kuwasiliana na wagonjwa. Hawezi kusema Kirusi. Hii ina maana kwamba hawezi kutambua magonjwa yanayowakumba wagonjwa ili kuweza kuwatibu ipasavyo. Zaidi ya hayo, habari za kuwasili kwa Mkaguzi Mkuu zinapomfikia, anawafukuza wagonjwa ambao hawajapata shufaa kutoka hospitali. Hii ni kwa sababu anataka Mkaguzi Mkuu amtambue kama kiongozi anayefahamu majukumu yake.

Bw. Hakimu naye hatekelezi wajibu wake vyema. Ofisi za mahakama ni chafu zimejaa kila aina ya takataka. Anachukua hongo na kutoa maamuzi yasiyokuwa ya haki. Anatueleza haya:

> **Hakimu:** …Nimekuwa nikikalia kiti cha hakimu hapa kwa muda wa miaka kumi na tano na kama ningepaswa kuzichunguza kumbukumbu za mahakama..naam, najiosha mikono yangu! Solomoni mwenyewe hangejua vipi kutofautisha ukweli na uwongo! (Uk. 11)

Karani wa mahakama naye ananuka vodka. Yeye huendesha kesi mahakamani akiwa mlevi aidha amezibadili ofisi za mahakama na kuzifanya kuwa vibanda vya kufugia kuku, bata na ndege. Isitoshe, hajawajibika katika kuhifadhi rekodi za mahakama. Bw. Posta ni mhusika mwingine ambaye hajawajibika katika kushughulikia barua za wateja wake. Yeye huzifungua na kuzisoma. Akipata zile zilizo na tetezi zozote kuwahusu anazihifadhi.

Kwa upande mwingine, Diwani I na Diwani II na Mhubiri wamekosa kuwajibika kama washauri wa Meya. Badala ya kumkosoa, wanampotosha. Wanakubaliana kuwepo kwa nyongeza na marupurupu ya walinda usalama, kutotozwa kodi kwa madiwani na nyongeza ya mishahara kwa madiwani. Washauri hawa hawawazii kuwa Baraza halimudu kutoa malipo haya kwani tayari lina upungufu wa fedha. Isitoshe, Diwani II anapendekeza uundwaji wa kamati za Baraza, ambazo hazina umuhimu wowote kwa Baraza ila wanataka kuzitumia kulifisidi. Aidha, Mhubiri ambaye ni kiongozi wa dini

ameshindwa kutekeleza wajibu wake ipasavyo. Anafahamu kuwa Mstahiki Meya anawadhalilisha raia. Badala ya kuukosoa uongozi wake, anaendelea kuuombea udumu milele kwa kuwa anafaidika kutokana na sadaka ya laki moja anayolipwa kila mwezi.

Mifano hii na mingine inachangia katika kupevua kauli kuwa tamthilia hizi mbili zinaingiliana kimaudhui. Aidha, maudhui ya ukosefu wa uwajibikaji yameendelezwa kwa kina katika tamthilia zote mbili na hivyo kuingiliana na kuchangizana.

### 5.4 Unafiki

Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* zinaingiliana katika kudhihirisha maudhui ya unafiki. Mkuu wa Wilaya anajifanya ameokoka lakini matendo yake ni mabaya. Anawadhulumu na kuwanyanyasa wafanyibiashara. Anamshauri Bw. Hakimu aokoke ilhali yeye mwenyewe hajabadilishwa na hiyo dini anayojaribu kueneza. Aidha, anamweleza Ghlestakovu kuwa ametembea hotelini kwa sababu ya upendo wa Yesu alio nao kwa wasafiri kuhakikisha kuwa wamepokelewa vyema. Ukweli ni dhahiri. Amefika pale hotelini kutafuta njia ya kumhonga. Zaidi ya hayo, anajifanya kuwa yeye hataki sifa kutoka kwa mtu yeyote ilimradi tu mji unatunzwa vyema, mitaa safi na wafungwa wanatunzwa. Huu ni unafiki kwa kuwa tunafahamu kuwa hajatekeleza anayomweleza Ghlestakovu.

Mstahiki Meya naye anajidai kuwa amekuwa akihisi kuwa angeiacha kazi yake ya umeya ili aweze kuungana na Mhubiri kueneza injili. Haya yalikuwa tu ni maneno aliyonuia kumshawishi Mhubiri ili aendelee kuunga mkono utawala wake. Meya anasema:

> **Meya**: (Kwa mhemko). Umenigusa ndugu mhubiri kila tukikutana kitu kutoka ndani kabisa hunisukuma kutaka nikufuate. Mara mbili hivi karibu niache kazi hii nije tushirikiane. (Uk. 41)

Mhubiri badala ya kumkosoa Meya anamuunga mkono. Anaendelea kuombea uongozi unaomdhulumu mwananchi udumu milele. Anakubali kuwa atakuwa akienda kuliombea Baraza mara moja kwa juma. Baraza nalo litakuwa linagharamia usafiri wake na kumtolea sadaka ya shilingi laki moja kila mwezi. Anamsisitizia Meya kuwa uongozi unaofuata dini utadumu milele kwa vile umebarikiwa. Hii ni hila ya kumfurahisha Meya ili aendelee kutoa sadaka. Pia anamwahidi katika maombi kuwa hakuna atakayemchezea lakini baadaye tunaona Meya akishtuliwa na mgomo wa wafanyikazi na mwishowe anaachishwa kazi.

Mstahiki Meya anajifanya kuwa kiongozi bora. Anasema kuwa ni kutokana na jinsi ambavyo alikuwa ameudhibiti uongozi wa Baraza la Cheneo ndivyo ameweza kuchaguliwa kwa mara ya tatu mfululizo. Ili kumdhihirishia Daktari Siki kauli hiyo, anamwita mpambe wake Gedi na kumtuma kwa mhazili wake. Anamtaka apange jinsi ambavyo nyimbo za kizalendo zingeweza kuchezwa katika idhaa ya Baraza. Hatua zote hizi ni za kinafiki. Lengo la haya yoye ni kuwafumba watu macho ili aweze kuonekana mzalendo machoni pa wakazi wa Cheneo.

Aidha, katika kikao, madiwani wanapendekeza kuandaliwa kwa mashindano baina ya vijana. Inavyojitokeza ni kuwa mashindano hayo yangeweza kupeperushwa katika vyombo vya habari. Kiundani, hii ni njia ya udanganyifu ambayo Meya anatumia kuimarisha kukubalika kwake na umma. Diwani II ambaye ni mmoja wa vibaraka wake anasema kuwa kuonyeshwa kwa mashindano haya kwenye vyombo vya habari, kungeleta uzalendo miongoni mwa wanacheneo. Anasema: "Uzalendo utawamiminikia watu katika pembe zote za Cheneo." (Uk. 20)

Isitoshe, Mstahiki Meya anamwamrisha Diwani III kuhakikisha kuwa madiwani hawatozwi kodi. Hii ni kwa sababu diwani huyu alikuwa akisimamia kitengo cha uchumi na kazi. Hata hivyo, kwa kuwa anafahamu changamoto ambazo wakazi walikuwa wakipitia, anapinga agizo hilo. Kwa upande wake, Meya anashikilia kuwa hiyo ni demokrasia. Japo anatumia mabavu kuona kuwa amri zake zinafuatwa, anaifanya ionekane ni uamuzi wa wengi. Wanapotamatisha kikao Meya, Diwani I na Diwani II wanaitikia kauli yao ya Cheneo idumu milele. Kauli hii inaashiria wanajali Baraza lakini si kweli. Ni unafiki tu.

Zaidi ya hayo, Mstahiki Meya anajifanya mtu mzuri hasa wakati wa uchaguzi unapokaribia kama njia ya kujihakikishia ushindi. Anasema kuwa hangetaka kusikia visa vya watu kufa wakati huu. Hataki vifo hivyo vimletee kisirani katika maazimio yake ya kupata kura kutoka kwa wananchi.

Bw. Huruma na madiwani ni viongozi wengine ambao wanadhihirisha maudhui haya ya unafiki. Bw. Huruma anawafukuza wagonjwa kutoka hospitalini. Wamebaki kumi tu. Anataka kupata sifa bora kutoka kwa Mkaguzi Mkuu. Aidha, anajifanya rafiki mwaminifu kwa Mkuu wa Wilaya. Anakwenda kwake kumpongeza baada ya kupata habari za kuposwa kwa bintiye ingawa anamchukia, kumdharau na kumwona kama mtu duni asiyefaa uongozi.

Kwa upande mwingine Diwani I na Diwani II wanaonyesha unafiki. Wanapanga namna ya kulilaghai Baraza rasilmali zake kwa kuuza fimbo ya Meya ng'ambo ili wajilipe kwa kazi ambayo si halali. Aidha, Diwani I ananuia kuwatangazia watu kuhusu kujitolea kwa Baraza la Cheneo kutetea demokrasia na uhuru waa kujieleza. Hili litakuwa tamko la Baraza linalonuiwa kuwapoza raia baada ya kupigwa na askari wa Baraza. Zaidi ya hayo, Diwani I anampendekezea Diwani I1 kuandaa tamasha ya vijana kushindania zawadi kwa kubuni na kucheza nyimbo. Hii ni hila inayonuiwa kuwafanya vijana kuhisi kuwa wanathaminiwa kwa kutunikiwa zawadi na kuonyeshwa kwenye vyombo vya habari.

Ghlestakovu na Bili ni wahusika wengine ambao wanadhihirisha unafiki. Ghlestakovu anapogundua kuwa Mkuu wa Wilaya amekosea na kumdhania kuwa mtu mashuhuri kutoka Pitasbag, anapata ujasiri wa kumlaghai pamoja na maofisa wa idara mbalimbali. Anaomba mikopo kutoka kwa Mkuu wa Wilaya, Bw. Hakimu, Bw. Huruma, Mratibu wa Elimu na wafanyibiashara, anawadanganya kuwa yeye ni mwandishi wa michezo ya kuigiza na anajifanya kushikilia cheo cha juu huko Pitasbag kinachomwezesha kuhusiana na mawaziri, Mabalozi wa nchi mbalimbali na viongozi wakuu serikalini. Aidha, anajifanya kumposa bintiye Mkuu wa Wilaya. Baada ya kuwachezea shere viongozi hawa anatoweka.

Kwa upande mwingine, Bili anamshauri Mstahiki Meya kufanya *gentlemen*'s *agreement* na mwanakandarasi, anazua mpango wa kuiba fimbo ya Meya aidha anamshauri Meya dhidi ya kusikiliza kilio cha wafanyikazi. Anamweleza kuwa kilio chao ni kama cha chura kisichoweza kumzuia ng'ombe kunywa maji. Maji yanapozidi unga barazani, Bili anatoweka na kuzima simu. Meya anamtafuta asimpate. Isitoshe, anawashauri madiwani kuwa baada ya kutumia silaha kukabiliana na wafanyikazi waliokuwa wanagoma, wanapaswa kutafuta jinsi ya kuhakikisha kuwa sifa zao haziharibiki. Swala hili lilikuwa muhimu hasa kwa sababu ya wageni ambao wangewatembelea. Kusisitiza maneno yake anasema: "Sote tunajua umuhimu wa kuuma na kuvuvia." (Uk.61). Hii ina maana kuwa madiwani walikuwa na njia za kujionyesha kuwa viongozi wema japo walikuwa waovu.

### 5.5 Ufisadi

Gogol na Arege wanaendeleza maudhui ya ufisadi kwa njia zinazolandana. Mkaguzi Mkuu na Mstahiki Meya ni viongozi wafisadi. Mkuu wa Wilaya anapokea hongo kutoka kwa wafanyibiashara aidha anatoa zabuni za serikali kwa wafanyibiashara ambao wanamhonga. Zaidi ya hayo, anapora pesa zilizotolewa na serikali kuu kujenga kanisa la hospitali.

Kwa upande mwingine, Mstahiki Meya naye anashiriki ufisadi. Anauza vipande vya ardhi ambavyo anajipatia kwa njia ya kulaghai. Inavyojitokeza, miongoni mwa wanaonufaika na unyakuzi wa ardhi ni rafikiye Bili. Aidha wawili hawa wanaonekana wakijadiliana kuhusu vile ambavyo wangeweza kujipatia fedha kwa njia za ufisadi. Mstahiki Meya anamwambia kuwa anahitaji kumtimua mtu fulani aliyekuwa amepatiwa kandarasi na Meya aliyekuwa akiongoza kabla ya Mstahiki Meya. Kwa kina, wanajadiliana kuhusu vile wangeweza kujipatia fedha kutoka kwa mwandakarasi kwa kutumia njia za kilaghai.

Aidha, Mstahiki Meya anatumia fedha za umma kumpeleka mkewe ng'ambo kujifungua, anatumia mamlaka aliyopewa na katiba kuidhinisha nyongeza ya mishahara ya madiwani, anaidhinisha nyongeza ya mishahara na marupurupu ya walinda usalama ili waendelee kumuunga mkono, anaidhinisha malipo haramu kwa Bili kwa huduma asiyotoa, anaidhinisha kulipwa kwa ovataimu kwa Diwani I na Diwani II licha ya kwamba wamo katika mkutano wa kupanga jinsi ya kulifisidi Baraza, madiwani wanahongwa kwa kutotozwa kodi, kuongezwa mishahara na kuwekwa katika kamati mbalimbali ili watoe uamuzi wa kumpendelea Meya aidha anamhonga Mhubiri ili amwombee kwa kuahidi kugharamia petroli ya kumleta barazani na kumrudisha nyumbani na kumlipa shilingi laki moja kila mwezi. Hali kadhalika, mhazili wa Meya hakustahili kupata kazi anayoifanya lakini Meya anampigania mpaka anaipata.

Hakimu na Madiwani pia wanadhihirisha ufisadi. Hakimu anapokea hongo ya vijibwa kutoka kwa watuhumiwa. Aidha amepanga kujinufaisha kutokana na kesi inayowakabili Cheptovichi na Valinski. Amepanga kulipeleka jibwa lake kuwinda katika bustani ya Cheptovichi siku moja na Valinski na siku ya pili pia anamhonga Ghlestakovu kwa kumpa shilingi mia nne.

Madiwani nao wanapanga njama ya kuiba na kuuza fimbo ya Meya kujilipa ovataimu ambayo hawastahili. Aidha, wanapanga njama za kunufaika kutokana na hazina ya Baraza. Wanabuni kamati za madiwani ili kupata upenyu wa kuendelea kulifisadi Baraza huku wakiungwa mkono na madiwani. Tazama maongezi haya kati ya madiwani.

> **Diwani II**: Asilimia sabini ya madiwani wakiwa na kamati za kuhudumu watatuunga mkono na kulipunguza joto lilipo.
>
> **Diwani I:** Haswa! Wale wenye ushawishi zaidi wanaweza kuteuliwa kuongoza kamati hizo. Mstahiki Meya, uwezo unao. Katiba ya Cheneo inakupa mamlaka tosha kubuni kamati nyingi apendavyo na kuteua viongozi wake. (kwa upole) Kwa unyenyekevu tunakuomba kutumia mamlaka hayo.(Uk. 21)

Aidha, madiwani hawa wanataka kulipwa ovataimu na marupurupu kwa kushiriki katika kikao cha kuweka mikakati ya jinsi ya kuiba mali ya Baraza.

**5.6 Uchafuzi wa mazingira**

Tunaelezwa kuwa miji yote miwili inanuka uvundo. Takataka zimetapakaa kila mahali. Katika tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* tunaelezwa kuwa barabara za mji hazijafagiliwa na kuna rundo la takataka karibu na ua ya mshona viatu. Jiji la Cheneo nalo limechafuliwa sana. Uchafu umerundikana kila mahali mjini. Hata barabara iliyo nje ya ofisi ya Meya ina takataka nyngi zinazonuka uvundo. Meya anapopewa maji akiwa ofisini anashindwa kuyanywa. Harufu kutoka nje inamfanya adhani kuwa maji ndiyo yananuka. Mpambe wake Gedi anamfahamisha kuwa harufu hiyo ni ya takataka. Kwamba hewa ndiyo imebadilisha mkondo wake na harufu ya uozo kuelekea humo ofisini.

Mazingira ya hospitali ni machafu. Hospitali katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ni chafu mno. Mavazi na makazi ya wagonjwa ni machafu, hayajasafishwa kwa muda mrefu. Zahanati ya mji wa Cheneo inanuka uvundo. Waridi anamlalamikia jinsi ambavyo mazingira ya hospitali yalikuwa yamechafuka. Anasema kuwa hata maji ya kuosha yalikuwa hayapo. Nzi walikuwa kila mahali. Hali mbaya ya kikazi ndiyo inayomshinikiza Waridi kuacha kazi. Hata Diwani III anapozungumza na Daktari Siki, anakubali kuwa tangu wafanyikazi wagome mji umechafuka kupindukia. Kulikuwa na harufu mbaya kila mahali.

Wawakilishi wa wafanyikazi wanapokwenda kuwasilisha malalamiko yao kwa Meya wanasisitiza jinsi mazingira yalivyokuwa yamechafuliwa. Tatu, mmoja wa wawakilishi wa wafanyikazi anasema kuwa hata uvundo utawazuia watu kuingia mjini. Anaeleza vile ambavyo vyoo vilikuwa vichafu na kutishia kuzuka kwa maradhi ya kipindupindu. Hata Meya mwenyewe anakubali kuwa hali ya mazingira ilikuwa mbaya.

Kwa jumla, tamthilia hizi mbili zinaingiliana na kuchangizana kwa kina katika kukuza na kuendeleza maudhui ya uchafuzi wa mazingira.

**5.7 Migogoro**

Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* zinaingiliana katika kuendeleza maudhui ya migogoro. Mkuu wa Wilaya ni kiongozi anayewadhulumu na kuwakandamiza raia. Anawalazimisha wafanyibiashara kuchanga kilo hamsini za nta na kumpa zawadi wakati wa sikukuu. Iwapo wanakataa, anawatumia polisi ambao wanawapiga, kuwavuta videvu na kutishia kufunga maduka yao. Wafanyibiashara wanapopata habari kuhusu kuwasili kwa Mkaguzi Mkuu wanakwenda pale na kuwasilisha malalamiko yao. Baadaye wanashutumiwa na kutukanwa na Mkuu wa Wilaya kwa kuthubutu kutoa manung'uniko dhidi yake. Aidha, kuna mgogoro baina ya tajiri mwenye hoteli na Ghlestakovu. Mgogoro huu unasababishwa na deni analojilimbikiza Ghlestakovu. Anakula na kulala katika hoteli bila kutoa malipo.

Kwa upande mwingine, Mstahiki Meya ni kiongozi anayetawala kwa mabavu, hila na ulaghai. Utawala wake unaibua matatizo mengi sana barazani. Migogoro mingi inazuka. Kwa mfano, kuna mgogoro mkubwa baina ya wafanyikazi na viongozi. Mgogoro huu unatokana na tabia ya viongozi ya kujilimbikiza mali huku wakisahau maslahi ya wafanyikazi. Wafanyikazi wanakumbwa na matatizo mengi kama vile vifo vinavyotokana na ukosefu wa matibabu, kupanda kwa gharama ya maisha na mishahara duni inayobakia pale pale huku viongozi wakijiongezea mishahara na pia kupitisha kanuni ya kutolipa kodi. Zaidi ya hayo, wafanyikazi hawa wanafanya kazi katika mazingira duni. Hawana vifaa muhimu vya utendakazi. Mambo haya na mengine yanasababisha kugoma kwa wafanyikazi. Hata katika mgomo wao, malalamiko yao hayashughulikiwi. Meya hataki kuwapa nyongeza ya mishahara, anasisitiza kuwa Baraza halina fedha.

Mgogoro mwingine unahusu hali ya wananchi kukosa huduma za kimsingi kama vile

dawa hospitalini. Wagonjwa wanaolazwa hospitalini wanahitajika kulipia kitanda bila matibabu. Aidha, uchafu unakithiri pale hospitalini kutokana na ukosefu wa maji. Wauguzi wanalipwa mishahara nusu kutokana na uhaba wa pesa. Wametamauka kutokana na hali hii ya mambo na baadhi yao wamejiuzulu. Kuna mgogoro kati ya Meya na Siki. Huu unatokea pale ambapo Siki anakuja kumtembelea Meya ili kulalamikia ukosefu wa dawa hospitalini pamoja na kumweleza matatizo mengine yanayowakumba wafanyikazi. Meya analalamika kuwa Siki amekuwa akichochea wafanyikazi kushiriki mgomo. Kwa kuwa Meya hataki kuelezwa ukweli, anamwita Gedi na kumwamrisha amtoe nje. Gedi pia anashauriwa kuhakikisha kuwa Siki haingii tena nyumbani kwa Meya. Zaidi ya hayo, tunapata mgogoro baina ya Meya na Diwani wa III. Meya anamtaka awape madiwani nyongeza ya mishahara kwa kuwa yeye ndiye anayesimamia kitengo cha uchumi na kazi. Diwani III anapinga vikali pendekezo hili. Anaeleza kwamba Baraza lina nakisi ya shilingi milioni mia moja na ishirini. Anataka madiwani wasubiri hadi uchumi utakapoimarika ndipo waweze kupata nyongeza pamoja na wafanyikazi wengine wa Baraza. Wawili hawa pia wanatofautiana kuhusu jinsi ya kusuluhisha matatizo ya wafanyikazi. Diwani III anapinga njama za Meya, Diwani I na Diwani II za kuinua  kiwango cha uzalendo kupitia kwa propaganda aidha anapinga pendekezo la uundwaji wa kamati za madiwani kwa kusema kwamba huenda zisiwe na umuhimu wowote kwa Baraza. Kwa sababu ya upinzani huu, ametengwa na madiwani wengine ambao wanamtazama kama kibaraka kwa kutetea haki za wanyonge.

### 5.8 Utabaka

Jamii za *Mstahiki Meya* na *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* zimegawika katika matabaka. Kuna tabaka la matajiri na la maskini. Jamii ya Cheneo imegawika katika matabaka mawili: la viongozi matajiri na jingine la maskini. Maskini wanawakilishwa na wafanyikazi wa Baraza kama vile mamake Dadavuo Kaole. Mama huyu ana mtoto mgonjwa. Anasema kuwa mtoto alianza kuendesha baada ya kula kiporo kilichotoka kwa Meya. Hiki ni chakula ambacho huko kwa Meya kinatumiwa kulisha mbwa. Kidogo anachopata mama, anampa mtoto wake kikiwa baridi. Hana pesa za kununulia mafuta au makaa ili aweze kukichemsha. Hii ni ishara tosha kuwa Meya alikuwa wa tabaka la juu naye mama alikuwa wa tabaka la chini. Ni dhahiri pia kuwa wafanyikazi wa Mstahiki Meya walichukuliwa kama mbwa. Dida hajivunii kazi yake ya utumishi wa nyumbani kwa Meya. Anasema kuwa anadhalilishwa na kutukanwa na bwana wake.

Mstahiki Meya anamwambia rafikiye Bili kuwa mkewe alikuwa ameenda ng'ambo kwa sababu mbili: Kwanza, alikuwa ameenda kuwaona watoto ambao wanasomea huko. Meya mwenyewe anakiri kuwa watoto wake hawawezi kusomea nchini kwani viwango vya elimu vilikuwa duni. Hili ni jambo la kusikitisha sana hasa ikizingatiwa kuwa Meya na wenzake ndio walikuwa na jukumu la kuboresha viwango vya elimu. Elimu duni inayotolewa katika jiji la Cheneo ndio wanaopokea watoto wa wafanyikazi wanyonge. Hawa hawana uwezo wa kifedha wa kuwapeleka watoto wao ng'ambo. Pili, mke wa Meya ameenda kujifungulia huko. Meya anamwambia Bili kuwa madaktari wa Cheneo ni wa kubahatisha. Anadai kwamba hataki kubahatisha kujifungua kwa mke wake. Wafanyikazi wa kawaida hawawezi kumudu gharama hii. Hivyo basi, maisha yao yalikuwa ni ya kubahatisha. Wao pamoja na watoto wao wanakufa kwa kukosa matibabu. Tunaelezwa kuwa mtoto wa Kerekecha anafia mikononi mwake aidha mtoto wa shangazi ya Waridi naye anakufa. Ukweli ni kwamba kutowajibika kwa viongozi wa jiji ndiko kunakozorotesha hali za hospitali. Hawa ndio hawahakikishi kuwa mazingira ya hospitali ni mazuri.

Isitoshe, matajiri wanawapeleka watoto wao shuleni kwa magari makubwa makubwa yenye *air conditioner*. Watoto wa maskini wanatembea kwa miguu kwenda shuleni na wafikapo huko walimu wanawatimua kwa kukosa kulipa karo. Zaidi ya hayo, wafanyikazi wa Baraza wanaishi katika mabanda yaliyoinama na kuinamiana huku matajiri wakiishi katika makasri yaliyopambwa kwa mazulia yaliyonunuliwa kutoka ng'ambo.

Aidha, Beka ambaye ni mmoja wa wawakilishi wanaotetea maslahi ya wafanyikazi anaonyesha mvutano wa kitabaka anapolalamikia Meya kuhusu nyongeza ya mishahara. Huu ni wakati ambapo wawakilishi wa wafanyikazi wa kiwango cha chini walikuwa wameenda kwa Meya kulalamikia hali yao ngumu ya maisha. Anasema kuwa mara ya mwisho waliongezewa vipeni vichache. Wakati huo nao madiwani walipata nyongeza kubwa. Hali kama hii inaendelea kupanua pengo kati ya viongozi matajiri na wafanyikazi wachochole.

Kwa upande huo mwingine, utabaka unadhihirika katika *Mkaguzi Mkuu wa Serikali.* Matajiri wanawakilishwa na wahusika kama vile Mkuu wa Wilaya, Bw. Hakimu, Mratibu wa Elimu na Bw. Huruma ambao wanaishi katika majumba makubwa yaliyo na vyumba vya kuwakaribishia wageni. Tunaelezwa kuwa Mkuu wa Wilaya anaishi katika

jumba kubwa pia ana mtumishi anayepika na kunadhifisha nyumba. Nao Dob na Bob ni makabaila ambao wanamiliki mali na maduka ya kukodisha mjini. Makabwela nao wanawakilishwa na Mishka, Yosif na mpishi hotelini. Hawa wanaishi maisha duni ya kuwatumikia mabwanyenye. Kwingineko, tunaelezwa kuwa mke wa Sajeni anadhulumiwa kwa sababu yeye ni mnyonge aidha Mhunzi anashurutishwa kujiunga na kikosi cha wanajeshi kwa sababu hana chochote cha kumhonga Mkuu wa Wilaya.

## 5.9 Hitimisho

Katika sura hii, tumeendeleza uhakiki wa kimwingilianomatini katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya*. Katika mjadala wetu tumeona kuwa tamthilia hizi zinaingiliana katika kuyakuza na kutaendeleza maswala anuwai katika jamii. Waandishi Gogol na Arege wameshughulikia maudhui ya uongozi mbaya, ukosefu wa uwajibikaji, unafiki, ufisadi, migogoro, dini na kadhalika.

Tumedhihirisha jinsi wahusika wakuu; Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya wanavyoendeleza uongozi mbaya. Viongozi hawa wanawadhulumu na kuwakandamiza wanyonge. Wanatumia ulaghai kujipatia mali na kuandama mbinu hasi za uongozi. Aidha tumeangazia maudhui ya ukosefu wa uwajibikaji na kutathmini namna tamthilia zote mbili zinavyochangizana katika kuyaendeleza maudhui haya. Tumejadili maudhui ya unafiki na tumeweza kudhihirisha namna viongozi hawa wanajifanya kuwa wameokoka kumbe ni mbwa mwitu waliovalia ngozi za kondoo. Isitoshe, tumetathmini maudhui ya ufisadi, uchafuzi wa mazingira migogoro na utabaka na tumeonyesha jinsi yanavyoingiliana na kuchangizana.

Kwa jumla, tamthilia hizi mbili zinaingiliana na kuchangizana katika kukuza na kuyaendeleza maudhui. Kadhalika, kuna maudhui mengine madogo madogo kama vile elimu, upendeleo, udikteta na kadhalika.

## SURA YA SITA

## HITIMISHO

### 6.1 Utangulizi

Katika sura hii, tumejadili kwa ufupi matokeo ya utafiti wetu. Tumefanya hivyo kwa kutoa muhtasari wa yale tuliyotekeleza na kuyaibua katika uchunguzi huu kwa kurejelea madhumuni na maswali ya utafiti. Pamoja na hayo, tumehitimisha kazi yetu kwa kutoa mapendekezo ya utafiti katika mada ya mwingilianomatini.

### 6.2 Muhtasari wa matokeo

Katika utafiti wetu, tumehakiki na kutathmini swala la mwingilianomatini katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya*. Kwa mujibu wa utafiti wetu, tumegundua kwamba baadhi ya kazi za kifasihi huingiliana na kuchangizana. Hii ni kwa sababu fasihi ni kioo cha jamii na wasanii huchota malighafi yao kutoka jamii. Aidha, binadamu wote ulimwenguni hughasiwa na takribani maswala yanayofanana. Kwa hivyo, si ajabu waandishi tofauti kuandikia matukio yayo hayo kwa njia zinazolandana. Aidha tumeona ya kwamba tamthilia hizi mbili ziliandikwa na wasanii waliokulia katika mazingira na vipindi tofauti. Tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* ilichapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 1834 huku *Mstahiki Meya* ikichapishwa 2009, ingawa masafa ya muda baina ya kuchapishwa kwa kazi hizi ni mapana zaidi, tahakiki pevu inabainisha kwamba kazi hizi zinafanana kwa kiwango fulani. Hata hivyo, tumehakiki na kutathmini mwingiliano katika usawiri wa wahusika, ploti, mandhari, na hali kadhalika mwingiliano katika maudhui. Tumeigawa tasnifu katika sura tano:

Sura ya kwanza inahusu utangulizi wa utafiti. Katika sehemu hii tumeeleza maswala ya kimsingi ya utafiti wetu. Maswala hayo ni pamoja na: mada ya utafiti, tatizo la utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, sababu za kuchagua mada, upeo na mipaka ya utafiti, msingi wa kinadharia, yaliyoandikwa kuhusu mwingilianomatini na mbinu za utafiti.

Katika sura ya pili, tumetaja na kutoa fasili za vipengele mbalimbali katika mwanda wa kimwingiliano. Tumefafanua vipengele vya msuko na aina za misuko, wahusika na mbinu za kuwasawiri wahusika, mandhari, maudhui na dhamira.

Katika sura ya tatu, tumehakiki na kutathmini mwingiliano wa kiploti katika tamthilia za

*Mkaguzi Mkuu wa Serikali na Mstahiki* Meya. Tumeonyesha jinsi tamthilia hizi zinavyolandana kimsuko kufutia uhusiano wa karibu wa vitushi kiusababishi. Misuko yote miwili inahusu uongozi dhalimu na matumizi mabaya ya mamlaka ya viongozi Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya. Aidha, tumeonyesha jinsi tamthilia zote zilivyojaa migogoro inayomtia msomaji hamu ya kutaka kuzisoma.

Katika sura ya nne, tumehakiki na kutathmini mwingiliano wa kiwahusika. Waandishi Nikolai Gogol na Timothy Arege wametuandikia tamthilia ambazo kwa kiwango kikubwa zinashabihiana katika usawiri wa wahusika. Baadhi ya wahusika wanashabihiana katika sifa na mienendo. Mathalani Mkuu wa Wilaya na Mstahiki Meya kama wahusika wakuu, wanaingiliana kwa kiwango cha juu. Wote ni viongozi walio na vyeo vya juu zaidi katika maeneo wanayoongoza na kama ambavyo tumedhihirisha, viongozi hawa ni wafisadi, wamekosa busara na uwajibikaji, wanafiki, wenye ubinafsi, tamaa na kiburi, waoga pia wanaandama mbinu hasi za uongozi.

Bw. Hakimu na Diwani I ni wasimamizi wa idara. Viongozi hawa wanaiga tabia na mienendo ya wakubwa wao kazini. Idara wanazosimamia zimejaa uozo. Wote wanashiriki ufisadi wamekosa uwajibikaji na ni wanafiki wakubwa. Aidha, Bw. Huruma na Diwani II wanadhihirisha mwingiliano. Mbali na wahusika hao, tumeonyesha mwingiliano kati ya Yosif na Dida. Hawa ni watumishi wanaofanya kazi zao kwa bidii aidha ni wanyenyekevu na watiifu. Hali kadhalika, tumeonyesha mwingiliano kati ya vikosi vya polisi katika jamii zote mbili. Isitoshe, tumedhihirisha jinsi wafanyibiashara na wafanyikazi wanavyolandana. Wanadhulumiwa na kukandamizwa na viongozi wao. Mifano hii na mingine mingi inatudhihirishia kuwa tamthilia hizi mbili zinaingiliana kiwahusika. Isitoshe, tumeangazia swala la mandhari. Tumeona kuwa kazi za kifasihi huingiliana kimandhari. Matukio mengi hutokea katika mazingira yanayoshabihiana. Waandishi wote wawili wametusawiria mazingira sawa ya kijamii kama vile ofisini, nyumbani, hospitalini na kadhalika.

Katika sura ya tano, tumehakiki na kutathmini mwingiliano wa kimaudhui. Kwa mujibu wa utafiti wetu, tumedhihirisha kuwa kazi za kifasihi huingiliana kimaudhui. Takribani kazi zote za kifasihi huingiliana na nyingine katika kuangazia matukio anuwai katika jamii. Madai haya yanashadidiwa na mwingiliano wa kimaudhui katika tamthilia hizi mbili. Zote zinaangazia maswala ya uongozi mbaya, ukosefu wa uwajibikaji, unafiki, ufisadi, uchafuzi wa mazingira, migogoro, utabaka na kadhalika. Hii ni kwa sababu

wasanii huchota malighafi yao kutoka jamii aidha binadamu wote ulimwenguni hukerwa na takribani maswala yanayofanana.

## 6.3 Hitimisho

Katika kazi hii tulinuia kufanya mambo matatu. Kwanza, tulinuia kuonyesha mwingiliano wa kifani katika tamthilia ya *Mstahiki Meya* na *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*. Tumelionyesha hili katika sura ya tatu na ya nne. Pili, tulinuia kuonyesha mwingiliano wa maudhui. Tumedhihirisha hili kwa kutoa mifano jinsi tamthilia hizi zinaingiliana na kuchangizana. Tatu, tulinuia kuonyesha kuwa nadharia ya Mwingilianomatini inafaa katika uhakiki wa tamthilia ya Kiswahili. Tumedhihirisha hili kwa kuitumia kuhakiki na kutathmini vipengele vinavyoingiliana katika tamthilia za *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya*.

Aidha, tulikuwa na nadharia tete tatu. kwanza, tulichukulia kwamba baadhi ya matini za kifasihi huchangizana na kuingiliana kifani. Tumethibitisha nadharia tete hii kuwa na mashiko. Tumeona kuwa matini za kifasihi zinaingiliana na kuchangizana katika vipengele vya msuko, mandhari na wahusika.

Pili, tulichukulia kuwa tamthilia ya *Mkaguzi Mkuu wa Serikali* na *Mstahiki Meya* zinaingiliana kimaudhui. Tumedhihirisha kuwa nadharia tete hii ni ya kweli. Maudhui ya tamthilia hizi yanaingiliana.

Tatu, tulichukulia kuwa nadharia ya Mwingilianomatini inafaa katika kuhakiki tamthilia ya Kiswahili. Tumethibitisha hili kwa kuonyesha kuwa nadharia hii inafaa katika kuhakiki tamthilia ya Kiswahili. Aidha, hamna matini yoyote ya kifasihi ambayo inaweza kuangaliwa kivyake na kujitegemea.

Kwa jumla, tunatumai utafiti huu pamoja na tahakiki nyingine, utakuwa muhimu katika kuzihakiki kazi za kifasihi kimwingilianomatini.

## 6.4 Mapendekezo

Utafiti wetu umejikita katika vipengele vichache tu katika mwanda mpana wa kimwingilianomatini. Kwa hivyo, tunawapendekezea watafiti wa baadaye kuhakiki mwingilianomatini wakizingatia mtindo katika kazi tofauti. Kazi hizi zinaweza kuwa za waandishi wawili tofauti au zaidi. Aidha, mbinu za uashiriaji wa maana hazijatafitiwa vya kutosha na hasa kwa mujibu wa nadharia ya Mwingilianomatini.

Utafiti huu ni muhimu katika fasihi ya Kiswahili kwa sababu umetoa mchango mkubwa katika kuziba pengo lililokuwepo la uhakiki wa matini za kifasihi ya Kiswahili katika misingi ya nadharia ya Mwingilianomatini.

## MAREJELEO


Allen, G. (2000). *Intertextuality*.U.S.A and Canada: Routledge.

Arege, T. (2007). *Chamchela.* Kenya: Jomo Kenyatta Foundation.
(2009). *Mstahiki Meya*. Nairobi : Vide Muwa publishers.

(2009). *Kijiba cha Moyo.* Nairobi: Longhorn publishers.

Bakari, M.(2011). Usemezano kama mkakati wa kufahamu riwaya za *Babu Alifufuka*

(2001), *Bina-Adamu* (2002) na mkusanyiko wa hadithi fupi *Sadiki Ukipenda*

(2002). Tasnifu ya M.A. Chuo Kikuu cha Kenyatta. Haijachapishwa.

Bakhtin, M.(1981). *The Dialogic imagination. Four Essay, Austin*: University of Texas.

(1986). *Speech & Genres & Other late Essays*. Austin: University of Texas press.

(1990). *Art & Answerability*. Austin: University of Texas press.

Barthes, R. (1975). *The Pleasure of the Text*. New York hill & Wang.

De Saussure, F. (1983). *A Course in General Linguistics.* Lasalle: Open Court.

Forster, E.M. (1927). *Aspects of the Novel*. London: Penguin Books.

Genette, G. (1980). *Narrative Discourse: An Essay in Method.* Ithaca: Cornell University

Gogol, N. (1979). *Mkaguzi Mkuu wa Serikali*. (Tafsiri ya Christon Mwakasaka). Nairobi: East African Educational publishers Ltd.

Hussein, E. N. (1971). *Mashetani.* Dar es Salaam: Oxford University press.

Hyslop, G. (1957). *Afadhali Mchawi.* Nairobi: Oxford University Press.

(1957). *Mgeni Karibu.* Nairobi: Oxford university press.

Imbuga, F. (1976). *Betrayal in the city*. Nairobi: East African publishing House.

Kezilahabi, E. (1971). *Rosa Mistika*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.

(1974). *Kichwa Maji*. Nairobi: East African Publishing House.

(1975). *Dunia Uwanja wa Fujo.* Nairobi: East African Literature Bureau.

(1978). *Gamba la Nyoka*. Arusha: East African Publishing House.

(1990). *Nagona*. Dar e salaam; Dar es Salaam University press.

(1991). *Mzingile. Dar es Salaam*: Dar es Salaam University press.

Kithaka Wa Mberia. (2001). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba publications Ltd.

Kitsao, J. (1980). *Uasi*. Nairobi: Oxford University press.

Kristeva, J. (1990). *Desire in Language. A Semiotic Approach to Literature and the Arts.*Thomas Gora, Alice and Leon (Trans) New York. Columbia University Press.

Kuria, H. (1957). *Nakupenda Lakini*. Nairobi: East African Literature Bureau.

Mbatiah, A.M. (2001). *Kamusi ya Fasihi*. Nairobi: Standard Textbooks Graphics and publishing.

Mohamed, S. A. (1990). *Tata za Asumini*. Nairobi: Longhorn Publishers.

(1995). *Amezidi*. Nairobi: EAEP.

(2001). *Babu Alipofufuka.* Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

(2002). *Sadiki Ukipenda na Hadithi Nyingine*. Narobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Msokile M. (1993). *Misingi ya uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: East African Educational publishers Ltd.

Mugambi, J. M. (1982). "Uhakiki wa maudhui katika Tamthilia za Kiswahili za Kikenya zilizochapishwa". Tasnifu ya Uzamili Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Mzee, S. (1980). *Mkuki wa Moto*. East African Publishing House. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd. Nairobi: Vide Muwa publishers.

Ngugi wa Thiongo na Mugo, M. (1978). *Mzalendo Kimathi* (Tafsiri). Nairobi: Heinemann.

Ngugi, G. (1961). *Nimelogwa Nisiwe* na *Mpenzi.* Dar es Salaam: East African Publishing House.

Njogu, K. na Chimerah, R. (1999): *Ufundishaji wa fasihi: Nadharia na mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Njoroge, H. (2007) Mwingilianomatini katika riwaya za *Tata za Asumini na Rosa Mistika.* Tasnifu ya uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa).

Nzuki, P. (2003). "Mwingiliano wa Fani na Maudhui katika ushairi wa Kithaka wa Mberia."Tasnifu ya Uzamil*i*. Chuo Kikuu cha Nairobi. (Haijachapishwa)

Ochoki, J. (2005)." Sitiari, jazanda na mwingilianomatini katika *Nagona na Mzingile*". Tasnifu ya uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi: (hazijachapishwa).

Olali T. (2008). *Mafamba.*Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Osodo, F. (1979). *Hatari kwa Usalama.* Nairobi: Heinemann Press.

Plottel, J. na Charney, H. (1978). *Introduction to Intextuality New Perspective in Criticism.* New York: Literary Forum.

Ruflo, J. (1985). *Pedro Paramo*. NewYork: Grove Printers Limited.

Wafula, R. M. (1999). *Uhakiki wa Tamthilia: Historia na Maendeleo Yake*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (1990). *Nagona. Da es salaam*: Dar es Salaam University Press.

(1991)."*Nagona na Mzingile*: Kezilahabi's Metaphysics" *katika Kiswahili.* Juzuu 58. *Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.* Dar es Salaam.

(1991). *Wingu la Kupita*. Nairobi: Longhhorn publishers Ltd.

(1997). "Contemptus mundi and Carpe Diem Motifs in Kezilahabi's Works" katika *Kiswahili*. *Juzuu 60. Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.* Dar es Salaam.

(2002). *Bina-Adamu!* Nairobi: Phoenix Publishers.

(2002) . *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.

(2003). *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publications Ltd.

(2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. Nairobi: focus publications Ltd.

(2008). *Kanzi ya Fasihi* 1:*Misingi na Uchanganuzi wa Fasihi.*

(2011). *Kamusi Fafanuzi ya Methali.* Nairobi: Target Publishers.